# MATUMIZI YA NYENZO KATIKA UFUNZAJI WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA UMMA JIMBO LA NYANDARUA, KENYA

**KARIUKI PETER MWANGI**

**TASNIFI HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA ELIMU, MITAALA NA MBINU ZA UFUNDISHAJI, KITIVO CHA ELIMU, CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA**

**2017**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote ile katika chuo chochote kile.

Sahihi……………………………… Tarehe………………………………

Kariuki Peter Mwangi

EM19/S/5011/2012

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maasai Mara

Sahihi ………………… Tarehe……………………………………………

Prof. Edward Tanui

Profesa Mshiriki, Idara ya Mitaala na Usimamizi wa Elimu

Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Sahihi …………….. Tarehe………………………………………

Dkt Florence Miima

Idara ya Mawasiliano na Teknolojia

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**ABSTRACT**

Teaching process is a two – way communication between the teacher and pupils, and among the pupils themselves. Instructional media mediate and support such interactions. Utilization of instructional media in public primary school is crucial in teaching of Kiswahili. Therefore the study sought to investigate utilization of instructional media in teaching of Kiswahili in public primary schools of Nyandarua county, Kenya. The objectives were: To establish instructional media used in teaching of Kiswahili, to evaluate the level of utilization of instructional in teaching of Kiswahili in public primary school, to investigate the influence of instructional media in teaching of Kiswahili and to explore challenges encountered by teachers in utilization of instructional media. The study was guided by Media Richness Theory propounded by Daft and Lengel in 1986. The study adopted a descriptive design. The study targeted 331 public primary schools, 331 public school head teachers and 369 teachers teaching Kiswahili in class eight. Purposive sampling was used to select a sample of 46 schools and their head teachers. Simple random sampling was used to sample 55 teachers teaching Kiswahili in class eight. Collection of data was done through questionnaires. Data was analyzed through descriptive statistics which included tables, graph, and percentages. The study found out that instructional media has positive influence on teaching of Kiswahili, most schools have an acute shortage of instructional media in Kiswahili and teachers do not use instructional media while teaching Kiswahili. The study recommends the government and other stakeholders to oversee utilization of instructional media in Kiswahili through acquisition and distribution of instructional media and sensitizing teachers through seminars and workshops. It also recommends establishment of resource centers from grassroots to the national level. It is believed that the findings of the study will provide useful information to stakeholders in education on ways of improving teaching of Kiswahili through appropriate utilization of instructional media.

# IKISIRI

Ufundishaji wa somo lolote lile unajikita kwenye mawasiliano baina ya mwalimu na wanafunzi au kati ya wanafunzi wenyewe. Nyenzo za kufundisha huwa viungo muhimu wakati wa utoaji wa mafunzo. Utafiti ulichunguza matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya. Madhumuni ya utafiti yalikuwa: Kuainisha nyenzo zinazotumika kufundisha Kiswahili, Kutathimini kiwango cha matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, kubainisha athari za nyenzo katika utendaji wa wanafunzi na kubainisha changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo iliyoasisiwa na Daft na Lengel mwaka wa 1986. Muundo wa kimaelezo ulitumika. Sampuli lengwa ilikuwa ni shule 331 za msingi za umma, walimu wakuu 331, walimu 369 wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane. Mbinu ya kuteua sampuli kimakusudi ilitumika kuteua sampuli ya shule 46 pamoja na walimu wakuu wa shule hizo. Mbinu ya unasibu ilitumika kuteua sampuli ya walimu 55 wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane. Hojaji ilitumika kama kifaa cha kukusanya data. Data ilichanganuliwa kupitia kwa takwimu ya kimaelezo ambapo majedwali, grafu na asilimia zilitumika. Utafiti uligundua kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari chanya, shule nyingi zina upungufu wa nyenzo za kufundisha Kiswahili na walimu wengi hawatumii nyenzo za kufundisha Kiswahili. Utafiti unatoa mapendekezo kwa serikali na washikadau wa sekta ya elimu wahahakikishe upatikanaji na uenezaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma.Walimu wa Kiswahili wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili kupitia kwa warsha na semina; na vituo vya nyenzo za kufundisha Kiswahili vianzishwe kutoka mashinani hadi katika ngazi za kitaifa. Matokeo ya utafiti huu yatawafaa washikadau wengi katika sekta ya elimu nchini kwani yatawawezeshe kuimarisha ukusanyaji na maandalizi ya nyenzo ili kuboresha ufunzaji wa Kiswahuili.

## FAHARASA


IKIRARI....................ii
ABSTRACT .................... iii
IKISIRI....................iv
SURA YA KWANZA....................1
UTANGULIZI ....................1
1.1Utangulizi wa Sura ya Kwanza....................1
1.2 Usuli wa Utafiti....................1
1.3 Suala la Utafiti....................6
1.4 Lengo la Utafiti....................7
1.5 Madhumuni ya Utafiti ....................7
1.6 Maswali ya Utafiti ....................7
1.7 Umuhimu wa Utafiti ....................8
1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti ....................8
1.9 Ufinyu wa Utafiti....................9
1.10 Tahadhania za Utafiti ....................9
1.11 Ufafanuzi wa Istilahi....................10
1.12 VIFUPISHO....................11
SURA YA PILI ....................12
MAPITIO YA MAANDISHI ....................12
2.1Utangulizi....................12
2.2. Aina za Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.....................12
2.3. Kiwango cha Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Kiswahili....................13
2.4 Athari ya Matumizi ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Kiswahili. ....................15
2.5. Changamoto Za Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili....................20
2.6. Nadharia ya Utafiti....................21
SURA YA TATU ....................26
MBINU ZA UTAFITI....................26
3.1. Utangulizi....................26
3.2. Muundo wa Utafiti....................26
3.3. Eneo la Utafiti....................26

**3.4. Sampuli lengwa** .......... **27**
**3.5. Uteuzi wa Sampuli Kamili ya Utafiti** .......... **27**
**Jedwali 2: Uteuzi wa Sampuli ya Utafiti** .......... **29**
**3.6 Vifaa vya Utafiti** .......... **29**
3.6.1 Hojaji .......... 29
**3.7. Uthabiti na Uhalali wa Vifaa vya Utafiti** .......... **30**
**3.8. Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti** .......... **30**
**3.9. Majaribio ya Vifaa** .......... **31**
**3.10. Ukusanyaji wa Data** .......... **31**
**3.11. Uchanganuzi wa Data** .......... **32**
**3.12 Maadili ya Utafiti** .......... **33**
**SURA YA NNE** .......... **34**
**Uchanganuzi wa Data na Majadiliano ya Matokeo ya Utafiti** .......... **34**
**4.1Utangulizi** .......... **34**
**4.2 Usuli wa Watafitiwa** .......... **34**
4.2.1. Umri wa walimu wa Kiswahili .......... 34
4.2.2 Viwango vya elimu vya walimu wa Kiswahili .......... 36
4.2.3 Tajriba ya walimu wa Kiswahili. .......... 37
4.2.4 Idadi ya vipindi wanavyofundisha walimu wa Kiswahili kwa juma .......... 38
4.2.5 Ukaguzi wa hati za Kitaaluma .......... 39
**4.3 Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.** .......... **40**
4.3.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundisha Kiswahili .......... 42
**4.4 Viwango vya Matumizi ya Nyenzo za KufundishaKiswahili** .......... **43**
4.4.1 Mbinu Za Matumizi ya Nyenzo za kufundisha Kiswahili .......... 44
**4.5 Athari ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.** .......... **45**
**4.6 Changamoto za Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili** .......... **47**
**SURA YA TANO** .......... **49**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI** .......... **49**
**5.1 Utangulizi** .......... **49**
**5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti** .......... **49**
**5.3 Hitimisho** .......... **50**
**5.4 Mapendekezo ya Utafiti** .......... **51**
**5.5 Mapendekezo Kuhusu Utafiti wa ziada** .......... **51**

**MAREJELEO** ........ **52**
**VIAMBATISHO** ........ **56**
**KIAMBATISHO A** ........ **56**
**HOJAJI YA WALIMU WA KISWAHILI** ........ **56**
**KIAMBATISHO B** ........ **60**
**HEAD TEACHERS' QUESTIONNAIRE** ........ **60**
**KIAMBATISHO D** ........ **64**
**BARUA YA MAPOKEZI** ........ **64**

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 1: Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili Kuanzia Mwaka wa 2009-2012 katika Jimbo la Nyandarua…………………………………………………………...5**

**Jedwali 2: Uteuzi wa Sampuli ya Utafiti……………………………………………… 29**

**Jedwali 3: Umri wa Walimu wa Kiswahili.......................................................................35**

**Jedwali 4: Viwango vya Elimu ya Watafitiwa.................................................................36**

**Jedwali 5: Tajriba ya walimu wa Kiswahili.....................................................................38**

**Jedwali 6: Idadi ya Vipindi vya Kushughulikiwa na Walimu katika Juma.................39**

**Jedwali 7: Miitiko ya Walimu Wakuu Kuhusu Ukaguzi wa Hati za Kitaaluma .........40**

**Jedwali 8: Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.............................................41**

**Jedwali 9: Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundisha Kiswahili ........................................42**

**Jedwali 10: Njia Mbadala za Kufadhili Nyenzo za Kufundisha Kiswahili...................43**

**Jedwali 12: Athari ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundishia Kiswahili ........................46**

**Jedwali 11: Mbinu Za Matuimizi ya Nyenzo za Kufundishia Kiswahili ......................45**

**Jedwali 13: Changamoto Za Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili. .............47**

## ORODHA YA MICHORO

**2.7. Mgofu Dhanifu ........................................................................................................25**

## ORODHA YA GRAFU

**Grafu1: Viwango vya Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili .........................44**

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1Utangulizi wa Sura ya Kwanza

Sura hii inashughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, ufinyu wa utafiti, tahadhania za utafiti na ufafanuzi wa istilahi.

### 1.2 Usuli wa Utafiti

Ufundishaji ni mchakato unaohusisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi au kati ya wanafunzi wenyewe. Mawasiliano huhusisha mwanzilishi wa ujumbe, njia ya kupitisha ujumbe huo na mpokeaji wa ujumbe huo. Njia za upokeaji wa ujumbe huo hufanikishwa na kuwepo au kutokuwepo kwa nyenzo. Tukilinganisha na mazingira ya darasani, mwalimu kwa wakati mwingi huwa chanzo cha ujumbe, naye mwanafunzi huwa mpokeaji wa ujumbe huo. Ili mwanafunzi aupokee ujumbe kwa njia inayofaa, mwalimu hana budi kuitumia nyenzo kama kipatanishi kati ya ujumbe unaokusudiwa na mawazo ya mwanafunzi.Haya yakifanyika shabaha ya funzo itakuwa imelengwa. Kwa hivyo, nyenzo huathiri uelewa wa mwanafunzi kwa njia mbalimbali. Yapata karne mbili zilizopita, neno hili nyenzo lilitumika kumaanisha magazeti.Maana ya neno nyenzo kulingana na Mdee na Wenzake (2014) ni kuwa nyenzo ni vitu vya kutengenezea vitu vingine. Hivi sasa, isitilahi hii inajumulisha redio, video, tarakilishi, rununu, vifaa halisi, michoro, picha, kadi za maneno miongoni mwa nyingine.

Kwa mujibu wa Gathumbi na Ssebbunga (2005), nyenzo za kufundisha lugha ambazo humwathiri mwanafunzi huwa na sifa bia zifuatazo: Nyenzo ziweze kuvutia, ziweze kuingiliana vizuri na funzo, nyenzo ziwe za kukuza umbuji wa mwanafunzi na hatimaye ziweze kuingiliana vyema na maisha ya kawaida ya mwanafunzi. Gathumbi na Ssebbunga (2005), wanazigawa nyenzo za kufundisha katika makundi matatu. Makundi haya ni: Nyenzo za kusikilizwa na kutazamwa, nyenzo za kusikilizwa na nyenzo za kuonwa. Kulingana na wataalamu hawa, nyenzo za kusikilizwa/kuona hutumika katika ufundishaji wa sarufi. Kwa mfano, kadi za maneno hutumiwa kuandikia herufi kubwa ili kutoa msururu wa maneno katika hadithi. Picha kutoka kwa magazeti au za kamera, hutumika kufunzia herufi na miundo ya sarufi. Ndiposa Kongamano la Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA)

mwaka wa 2012, lilisisitiza uamilifu wa makala za *Taifa Leo* kama nyenzo za kufundishia Kiswahili. Nyenzo za kusikilizwa ni kama vile utepe na filamu. Nyenzo hizi hutumika kufundisha misamiati na sarufi ya lugha. Sehemu ya Sarufi ambayo hufunzwa kupitia kwa nyenzo hizi za kusikilizwa ni kama vile vihusishi vinavyoonyesha "chini ya"au "juu ya". Aina nyingine ya nyenzo za kufundisha ni ya kuonwa.Baadhi ya matumizi ya nyenzo za kuonwa ni kufafanua msamiati mpya. Nyenzo hizi huinua umakinifu wa mwanafunzi darasani. Mwanafunzi akimakinika, ufundishwaji wake katika Kiswahili utaimarika. Isitoshe, nyenzo za kuonwa husaidia kujenga kumbukizi za mwanafunzi. Kulingana na Baraza la Mitihani la Kenya (KNEC, 2015), katika karatasi ya kwanza ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili wa shule za msingi; hasa kuanzia swali la kumi na sita hadi la thelathini humtahini mwanafunzi lugha na matumizi yake. Sehemu hii humhitaji mwanafunzi kukumbuka vipengele vya lugha alivyofunzwa kama vile, methali, semi, takiriri miongoni mwa vingine.

Wringe (1995) aligawa nyenzo za kufundisha katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lile la nyenzo za kimapokezi, kwa vile vitabu, kadi za maneno, michoro, ubao mweusi au ukuta mweusi na chaki. Kundi la pili ni lile linalohusu nyenzo zinazohusisha teknolojia ya lugha. Mifano katika kundi hili ni aina za projekta, tepe za kurekodi na maabara ya lugha. Kundi la tatu kulingana na Wringe (1995) ni lile linalohusu teknolojia ya mawasiliano. Mifano ya nyenzo katika kundi hili ni kiyuweo, tarakilishi, rukono na mitandao.

Nyenzo huchukua mifumo mingi lakini kusudi kuu la nyenzo ulimwenguni ni moja. Kulingana na Flanders (1970), nyenzo ni njia ya kufanikisha mawasiliano. Katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ni sharti kuwepo na mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi wake. Mawasiliano haya hurahisishwa na huathiriwa zaidi na uwepo wa nyenzo za kufundisha.Zacharia (2012), anashauri kuwa matumizi ya vifaa vya kufundishi ni nyenzo muhimu sana kwa sababu zinatumika katika ujenzi wa maana katika funzo lolote lile; zaidi huwa msaada kwa mwalimu katika kumrahisishia kazi yake.

Edmenger (1979) akinukuliwa na Van (1984), anaorodhesha sababu za matumizi ya nyenzo za kufundisha. Baadhi ya sababu hizi ni kuwa, inamlazimu mwalimu afikiri kuhusu ujumbe anaokusudia kuuwasilisha kwa wanafunzi na njia ambayo ujumbe huo utapitia. Edmenger (1979) anazidi kusisitiza kuwa nyenzo hufikisha ujumbe kwa mwanafunzi kwa njia inayofaa bila utata wowote wa uelewa. Ukosefu wa utata wa uelewa utatoweka ikiwa kutakuwa na maingiliano mazuri kati ya funzo na mwanafunzi mwenyewe. Maingiliano haya

hufanikishwa na upatanisho bora wa funzo, nadharia, utendaji na nyenzo za kufundishi.Ellis (1991) anashauri kuwa nyenzo za kufundisha huwa daraja nzuri la upatanisho kati ya mwanafunzi na funzo lake. Haya yanaelezewa zaidi na nadharia ya Upatanisho iliyoasisiwa na Bruner (1966). Nadharia hii inaeleza kuwa ili ujifunzaji upatikane, lazima kuwe na maingiliano kati ya funzo na mwanafunzi. Bruner (1966) anazidi kufafanua kuwa, kunaweza kuwa na mtu wa kufanikisha maingiliano haya. Mtu huyu wa kati huchukua nafasi ya mwelekezi. Mwelekezi huyu, huwa tofauti na mwalimu wa kawaida. Yeye humsaidia mwanafunzi katika kutoa mwelekeo wa jinsi ya kulielewa funzo lake. Wakati mwingine nafasi ya mwelekezi huchukuliwa na nyenzo. Maelezo haya ya Bruner (1966) yanalingana na maelezo ya Ahrens (1980), anayesisitiza kuwa nyenzo humsaidia na humsimamia mwalimu.Tukiegemea maoni ya wataalamu Ellis (1991), Bruner (1966) na Ahrens (1980), utafiti ulitaka kuchunguza iwapo walimu wa Jimbo la Nyandarua wanatumia nyenzo za kufundisha Kiswahili ili kufanikisha maingiliano ya wanafunzi darasani.

Isitoshe, hapa nchini Kenya kuna masomo ya redio kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya walimu. Mafunzo haya huhusisha masomo yote ya shule za msingi kikiwepo Kiswahili.Vipindi hivi hutolewa na Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE). Vipindi hivi vya somo la Kiswahili kwa madarasa yote ya shule za msingi humsimamia mwalimu wa darasani na yamkini huwa na athari kuu kuliko ile ya mwalimu wa kawaida.

Ilinyenzo za kufundisha Kiswahili zimwathiri mwanafunzi katika ufunzwaji wake, ni lazima zitumike kwa utaratibu unaofaa. Chuo kikuu cha Missouri Kolumbia (2012), kiliorodhesha vipengele kumi na vitatu vya kufuatwa na walimu wakati wa uteuzi wa nyenzo za kufundisha. Baadhi ya vipengele hivi ni kuwa, mteuzi anashauriwa atafakari kuhusu kile anachodhamiria kukifunza kupitia kwa usaidizi wa nyenzo husika.Pili, mwalimu anashauriwa aitumie nyenzo kulingana na sifa bia za wanafunzi wake. Mfano wa sifa hizi bia ni uzoefu wa mwanafunzi katika matumizi ya kifaa husika.

Chuo Kikuu Cha Oldham (2012), kinathibitisha kuwa, nyenzo za kufundisha katika shule za Jimbo la Oldham, nchini Marekani huteuliwa na wataalamu wa Maktaba ya Nyenzo. Wataalamu hawahusaidiana na wazazi, wanafunzi na kitivo cha Nyenzo za kufundisha cha chuo hiki. Katika Chuo hiki Cha Oldham nchini Marekani, ni jukumu la kitivo cha nyenzo za kufunndisha kuandaa na kutoa mafunzo ya jinsi ya kuzitumia nyenzo. Wakati mwingine,

wazazi pamoja na wanafunzi hushirikishwa ili kutoa mapendekezo yao kuhusu nyenzo ambazo wangetaka zitumike kwenye maktaba ya chuo hicho. Utafiti ukichukua mikakati hii ya Chuo Kikuu cha Oldham kama timazi, ulitaka kuchunguza iwapo huwa na ushirikiano wa washikadau wa elimu katika kuteua na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

Baadhi ya madhumuni makuu ya kitivo cha nyenzo za kufundisha katikaChuo Kikuu cha Oldham (2012) ni kule kuinua usomaji wa burudani. Programu za tarakilishi ni mojawapo wa nyenzo zinazoinua hali hii ya usomaji wa burudani. Programu za tarakilishi ambazo huinua usomaji wa burudani zikijumulishwa katika ufundishaji wa Kiswahili huinua kiwango cha usomaji na usemaji wa mwanafunzi katika somo hili. Usomaji na usemaji huwa ni kati ya stadi muhimu sana ambazo hutahiniwa wakati wa kuyajibu maswali ya ufahamu katika mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili. Maswali haya huwa kati ya swali la 31 hadi la 50 katika mtihani wa karatasi ya kwanza ya Kiswahili KCPE. Hivyo basi, utafiti ulikusudia kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua hushirikisha wanafunzi katika programu za tarakilishi.

Utafiti ulilinganisha ufundishaji wasomo la Kiswahili na ule wa somo la Kiingereza. Ulinganisho huu ulipitia kupitia kwa maoni ya Schullstoim (1998), aliyedai kuwa nyenzo ni kiungo muhimu sana cha kufundisha Kiingereza kwa kuwa vifaa hivi huwezesha maingiliano ya mwanafunzi na maneno anayoyasoma kitabuni au ubaoni. Schullstoim (1998), anazidi kufafanua kuwa maingiliano mengine ni kati ya mawazo ya mwanafunzi na picha azitazamazo. Maingiliano haya yote hukuza uwezo wa mwanafunzi katika kusoma, kusikiliza, kufikiria, kuongea, kuandika, na kuwa na ustadi wa kutumia nyenzo na teknolojia. Ili kuinua stadi mbalimbali za lugha ya Kiswahili pamoja na maingiliano mengine ya mwanafunzi na funzo lake, utafiti ukiegemea maoni ya Schullstoim (1998) ulichunguza iwapo walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua hutumia nyenzo za kufundisha.

Hata hivyo, ukosefu wa nyenzo za kufundisha somo la lugha yoyote ile huwa na athari kwa mwanafunzi. Maoni haya yanaungwa mkono na Aduwa na Iyamu (2006) wanapodai kuwa ukosefu wa nyenzo za kufundisha somo la lugha yoyote hausababishi tu matokeo duni katika somo husika bali huathiri hata maendeleo yake katika somo la lugha. Madai ya Aduwa na Iyamu (2006) yanalingana na matokeo ya utafiti uliofanywa na Luvisa (2003) kuhusu upatikanaji wa nyenzo za kufunza sarufi ya Kiswahili katika wilaya ya Bungoma

uliyodhihirisha kuwa, shule nyingi nchini Kenya zinakabiliwa na uhaba wa nyenzo za kufundisha. Upungufu huu unaathiri ufaafu wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na matokeo yake yanadhihirika katika matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili.

Kulingana na madai ya Aduwa na Iyamu (2006) na matokeo ya utafiti wa Luvisa (2003), utafiti huu ulichunguza matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kati ya mwaka wa 2009 – 2012 katika Jimbo la Nyandarua. Matokeo haya yanaonyeshwa katika jedwali 1 lifuatalo:

**Jedwali 1: Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili Kuanzia Mwaka wa 2009- 2012 katika Jimbo la Nyandarua.**

| Kijimbo/mwaka | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Nyandarua Kaskazini** | 47.54 | 46.32 | 48.34 | 48.85 | **47.76** |
| **Nyandarua Kati** | 48.17 | 44.47 | 47.08 | 49.20 | **46.73** |
| **Mirangi-ini** | 47.66 | 49.43 | 48.97 | 48.67 | **48.68** |
| **Kipipiri** | 50.26 | 46.96 | 47.68 | 48.27 | **48.29** |
| **Nyandarua Magharibi** | 52.81 | 51.56 | 52.74 | 52.56 | **52.41** |
| **Nyandarua Kusini** | 51.73 | 49.22 | 47.68 | 50.47 | **49.78** |
| **Kinangop** | 54.39 | 50.89 | 51.67 | 52.55 | **52.38** |
| **Jumla** | **50.37** | **48.48** | **49.20** | **51.51** | **49.48** |

*Asili: Afisi ya Mkurugenzi wa Elimu Jimbo la Nyandarua(2013)*

Kutokana na jedwali 1, matokeo ya mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua yanahitilafiana. Vijimbo vya Kinangop (52.38) na Nyandarua Magharibi (52.41) vinatia fora kwa kuwa na alama ya wastani ya zaidi ya hamsini. Hiki ni juu ya kiwango cha wastani kinacholengwa na Baraza la Mitihani ya Kitaifa. Baraza hili hulenga asilimia hamsini kama alama ya wastani ya Kiswahili (KNEC, 2005).

Kijimbo cha Nyandarua ya Kati ndicho chenye alama ya chini zaidi kati ya vijimbo vyote saba. Hii ikiwa ni asilimia 46.73. Matokeo haya ni asilimia 3.27 chini ya alama ya wastani ya Baraza la Mitihani ya Kitaifa. Alama ya jumla ya Jimbo ni asilimia (49.48), ambayo ni chini ya alama ya wastani ya Baraza la Mitihani ya Kitaifa.

Wadau wa elimu katika Jimbo la Nyandarua wametoa sababu nyingi zinazochangia matoke haya duni.Baadhi ya sababu hizi ni ukosefu wa walimu wa kutosha, ukosefu wa ushirikiano kati ya walimu na wazazi na mitazamo hasi ya wanafunzi dhidi ya somo husika. Ukosefu wa matumizi ya nyenzo za kufundisha sio mojawapo wa sababu zilizotolewa. Utafiti unasadikisha kuwa matokeo ya mtihani wa kitaifa huwa mizani ya kupima jinsi nyenzo za ufundishaji zinavyoathiri ufundishaji wa somo la Kiswahili. Kulingana na maoni ya Schullstoim (1998), Aduwa na Iyamu (2006) na Luvisa (2003); utafiti ulitaka kuchunguza iwapo nyenzo za kufundisha zina umuhimu na athari yoyote katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

### 1.3 Suala la Utafiti

Matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa somo lolote lile nimuhimu kwa kuwa huwashirikisha wanafunzi katika shughuli mbalimbali za darasani na hata kuwawezesha kuelewa dhana ngumu na hatimaye kuimarisha matokeo yao katika mitihani ya kitaifa.

Ingawa wizara ya elimu na taasisi ya kukuza mitaala inapendekeza nyenzo mbalimbali za kushirikishwa kwenye ufunzaji wa mada mbalimbali, kuna madai kuwa, walimu wengi hawashirikishi nyenzo hizo katika shughuli zao za ufunzaji. Jambo kama hili linaweza kuchangia matokeo yasiyoridhisha.Matokeo ya Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua ni chini mno na mojawapo wa sababu zinazotolewa na washika dau ni kuwa mbinu zianazotumiwa na walimu zinachangia licha ya kuwa na ukosefu wa nyenzo. Hali hii ilimsukuma mtafiti kuchunguza ikiwa matumizi ya nyenzo katika kufundisha Kiswahili yana athari yoyote katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa ndani na nje ya nchi kuhusiana na nyenzo za ufundishaji. Matokeo ya tafiti hizi yamedhihirisha kuwa nyenzo za kufundisha zina umuhimu mkubwa katika kuimarisha matokeo ya mwanafunzi katika masomo mbalimbali. Utafiti ulikusudia kuchunguza kiwango cha athari za nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili. isitoshe, ilibainika kuwa utafiti wa aina hii haukuwa umefanywa hivi karibuni katika Jimbo la Nyandarua. Ni kutokana na uegemezi wa dhana hizi, ambapo, utafiti huu ulinuia kuchunguza matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

### 1.4 Lengo la Utafiti

Mawasiliano ni kipengee muhimu sana katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Mawasiliano haya huchangiwa na kuwepo kwa nyenzo za kufundisha kama ilivyothibitishwa na tafiti mbalimbali. Hivyo basi, lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza athari za matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

### 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

i) Kuainisha nyenzo zinazotumika na walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

ii) Kutathimini kiwango cha matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

iii) Kuchunguza athari ya matumizi ya nyenzo katika kuchangia matokeo bora ya Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

iv) Kubainisha changamoto za matuimizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

### 1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na na maswali yafuatato:

i. Je, kuna aina ngapi za nyenzo za kufundisha Kiswahili ambazo hutumiwa na walimu wa shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua?

ii. Je, nyenzo za ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua ni za kiwango kipi?

iii. Matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili huwaathiri vipi wanafunzi wa shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua?

iv. Je, kuna changamoto zipi zinazowakabili walimu wa shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua katika matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa washikadau wengi katika sekta ya elimu, hasa katika kuimarisha ufundishaji wa somo la Kiswahili. Washikadau hawa ni pamoja na walimu wakuu, walimu wanaofundisha Kiswahili, wanafunzi na wakuza mitaala. Utafiti utaboresha ufundishaji wa Kiswahili sio tu katika Jimbo la Nyandarua bali pia katika majimbo mengine nchini.

Walimu wakuu ndio wenye jukumu la kununua baadhi ya nyenzo za kufundisha. Mwalimu mkuu anawajibika kutambua nyenzo zinazofaakatika masomo mbalimbali.

Mwalimu anayefundisha Kiswahili ndiye mteuzi na mtumizi wa nyenzo. Naye mwanafunzihana budi kuifahamu nyenzo ili aweze kuitumia. Mara kwa mara mwanafunzi hushirikishwa katika kuitayarishanyenzo husika.

Wakuza mitaala, wanatarajiwa kutoa mwelekeo kuhusu nyenzo ambazo zinafaa kutumiwa na walimu wakati wa kufunza somo la Kiswahili. Mapendekezo yaohatimaye yanatarajiwa kuinua kiwango cha ufundishwaji wa mwanafunzi katika Kiswahili. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuwahamasisha walimu na wakuza mitaala kuhusu swala la matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.

Utafiti huu ulinuia kutoa mwelekeo ufaao kuhusu matumizi ya nyenzo za kufundisha ili kuyainua matokeo ya mwanafunzi katika somo la Kiswahili. Hatimaye, uchunguzi huu unatarajiwa kuchochea tafiti zaidi kuhusu uwanja huu mpana wa matumizi yanyenzo za kufundisha Kiswahili.

## 1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulijikita kwenye mada ya utafiti pekee ambayo ni matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, Jimbo la Nyandarua Kenya. Mada hii iliongozwa na madhumuni yafuatayo: Kuainisha aina za nyenzo zinazotumika katika ufundishaji wa Kiswahili, kutathmini kiwango cha matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, kuchunguza athari ya matumizi ya nyenzo za ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua na kubainisha changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.

Kwa upande mwingine, utafiti uliegemea miitiko kutoka kwa sampuli ya walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane katika shule za msingi za umma pekee pamoja na sampuli ya walimu wakuu ili kujumulisha matokeo ya utafiti.

Mtatifi hangeweza kudhibiti vibadiliki huru vya watafitiwa kama vile umri, kiwango cha elimu, na tajriba yao kwa kuwa matokeo yake tayari yamedhihirika. Utafiti ulijikita katika Jimbo la Nyandarua na uliangazia shule za msingi za umma pekee kwani inaaminika kuwa ndizo zinazofuata silabasi mpya ya mwaka wa 2002.

**1.9Ufinyu wa Utafiti**

Kuna mikakati mingi inayohusishwa ili kuinuamatokeo ya ufundishaji wa Kiswahili. Utafiti huu, ulishughulikia nyenzo za kufundisha kama kigezo kikuu cha kuimarisha matokeo haya.

Utafiti ulihusisha sampuli ya walimu wakuu wa shule za msingi za umma pamoja na sampuli ya walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane pekee kutoka katika Jimbo la Nyandarua.

**1.10 Tahadhania za Utafiti**

(i).Walimu wote wamefuzu na wana tajriba ya kufundisha somo la Kiswahili.

(ii) Walimu wote wanatumia silabasi mpya ya Kiswahili ya mwaka wa 2002.

## 1.11 Ufafanuzi wa Istilahi

**Kalibu:**Haya ni aina ya maswali ambayo mtafitiwa huteua miitiko kulingana na ukubalifu wake dhidi ya suala husika. Maswali haya huhusisha uteuzi kulingana na mizani ya Likert.

**Kiyuweo:** Kompyuta ndogo ya kupakata au kipakatalishi..

**Mgofu Dhanifu:** Mchoro unaoonyesha uhusiano kati ya vibadiliki huru na vibadiliki tegemezi vya utafiti.

**Nyenzo za kufundisha:** Hivi ni vifaa vyote vya kufundisha vinavyotumiwa na walimu ili kufikia malengo fulani ya funzo.

**Ufaraguzi:** Kutengeneza kifaa kwa kutumia vifaa vinavyopatikana kwa urahisi kutoka kwenye mazingira ya mwanafunzi ili kuokoa hali fulani ya kielimu.

**Ujifunzaji:** Upokeaji wa maarifa, ujuzi na mielekeo kupitia somo lolote lile likiwemo la Kiswahili.

## 1.12 VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BKM: | Baraza La Kitaifa La Mtihani |
| CHAKITA: | Chama Cha Kiswahili Cha Taifa |
| CBT: | Utowaji Wa Mafunzo Kupitia Kwa Tarakilishi |
| CBT: | Utowaji Wa Mafunzo Kupitia Kwa Tarakilishi |
| HZK | Nyenzo Za Kufundishia |
| JYK: | Jamhuri Ya Kenya |
| MBM | Mpango Wa Serikali Wa Masomo Bila Malipo |
| Mksm: | (KCPE) Mtihani Na Kitaifa Wa Shule Za Msingi |
| NUWN | Nadharia Ya Uwezo Wa Matumizi Ya Nyenzo (Media Richness Theory) |
| TEK: | Taasisi Ya Elimu Ya Kenya (Kie) |
| Ulk | Ujifunzaji Wa Lugha Za Kigeni |

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1Utangulizi

Sura hii inashughulikia mapitio ya maandishi ya utafiti. Mapitio haya ya maandishiyanagawika katika vijisehemu vifuatavyo: Aina za nyenzo zinazotumika na walimu katika ufundishaji wa Kiswahili, kiwango cha matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, athari ya matumizi ya nyenzo katika kuchangia matokeo bora ya Kiswahili, changamoto za matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, nadharia ya utafiti na mgofu dhanifu wa utafiti.

### 2.2. Aina za Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.

Nyenzo za kufundisha Kiswahili ni nyingi, lakini kwa mujibu wa utafiti huu nyenzo hizo zitagawika katika makundi matatu. Kulingana na Gathumbi na Ssebbunga (2005) ametaja aina hizo kuwa; nyenzo za kusikilizwa, nyenzo za kuonwa na nyenzo za kusikilizwa/kuonwa. Nyenzo za kusikilizwa ni zile zinazotoa sauti. Mifano ya nyenzo za kusikilizwa ni kama vile santuli, redio, tepu rekoda na maabara ya lugha (St Cloud, 2012). Kupitia kwa nyenzo za kusikilizwa, wanafunzi husikiliza na huiga matamshi bora. Nazo nyenzo za kuonwa kulingana na Finocchiaro (1993) ni kama vile ubao au ukuta mweusi, vitabu vya kozi, vifaa halisi, vifaa vya miigo, faili ya picha, chati, kadi za maneno na projekta. Bonono (1993) alipendekeza kuwe na faili ya picha kwa kila darasa katika shule zote za msingi. Picha hizi huongezea motisha na kuhimiza maana wakati wa kufanya mazoezi ya lugha za kigeni. Chuo kikuu cha St Cloud (2012) kinaongeza kuwa, nyenzo za kuonwa huhusisha matumizi ya macho. Deuter, Bradbery, & Turnbull(2015), wametoa mifano ya nyenzo za kuonwa zinazojumlisha picha, filamu, video na ramani. Mtaalamu Deuter na wenzake (2015) ameongeza kuwa nyenzo hizi za kutazamwa hutumika kama vifaa vya kufundisha.

Nyenzo za kutazamwa zina umuhimu mkubwa katika ufundishaji wa lugha. Huebener (1992) anadai kuwa katika ujifunzaji wowote ukiwemo wa lugha za kigeni, nyenzo za kuonwa huwa na dhima kuu, zaidi huwa ni njia ya kupatanisha hoja za funzo na mawazo ya mwanafunzi. Utumiaji wa nyenzo za kuonwa husaidia kuibua hali ambayo mwanafunzi humakinika kinyume na jinsi hali ingekuwa iwapo njia ya mdomo pekee ingetumika (Wright, 1989). Wright (1989) anasisitiza kuwa, nyenzo hizi za kuonwa hutumika vyema

kufundishavipengele muhimu vya lugha. Vipengele hivyo ni Kusikiliza, kuongea, kuandika, kusoma, sarufi na kaida za lugha.

Nyenzo za kuonwa hutumika kufundisha miundo ya lugha na misamiati ya Kiswahili. Miundo hii ni pamoja na fonolojia na mofolojia ya Kiswahili.Kwa mujibu wa Heinrich na Molenda (1993) kazi kuu ya kimsingi ya nyenzo za kuonwa ni kutumika mno kama kirejeleo cha kuonekana kuliko kirejeleo cha maongezi au maandishi. Nyenzo za kufundisha Kiswahili zikitumiwa kama kirejeleo cha kuonekana zitasaidia mwanafunzi kuelewa miundo ya lugha ya Kiswahili kwa kuwa dhana hii huwa dhahania.

Nyenzo za kusikilizwa/kutazamwa huhusisha kuona na kusikiliza (Kasbolah, 2003). Anderson na Krathwohl (2009) wanatoa mifano ya nyenzo za kusikilizwa/kuona kama ufundishaji kupitia kwa mitandao, kanda za televisheni na video, utoaji wa mafunzo kupitia televisheni, kanda za kunasia sauti na ipadi. Chuo kikuu cha St Cloud (2012) kinaongeza kuwa slaidi za filamu hupangwa kwa utaratibu kuelekezwa ukutani au kwenye kioo na kuwa njia mwafaka ya kufundisha lugha. Mbinu hii hutumika vyema katika kufanya mazoezi ya misamiati na miundo ya lugha ya Kiswahili. Mbinu hii humuondolea mwanafunzi uchovu na kuchochea motisha kwenye kipindi cha Kiswahili.

Aina za nyenzo za kufundisha ni nyingi. Utafiti huu ulichunguza kwa kina iwapo walimu wa Jimbo la Nyandarua hutumia aina hizi tatu za nyenzo za kufundisha ili kuboresha matokeo ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma. Isitoshe, uchunguzi ulidasi kuwepo kwa uwezekano wa matumizi ya nyenzo za kisasa kwa vile tarakilishi katika ufunzaji wa somo la Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.

### 2.3. Kiwango cha Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Kiswahili

Kufuatia dhima na umuhimu wa nyenzo za kufundisha Kiswahili, ni wazi kuwa zina majukumu makuu katika ufundishaji wa kiswahili. Uteuzi wa nyenzo za kufundisha unafaa ufanywe kwa utaratibu ufaao. Chuo Kikuu cha Missouri-Kolumbia (2012) kimeorodhesha vipengele kumi na vitatu vya kuzingatiwa na walimu wakati wa uteuzi wa nyenzo za kufundishia. Baadhi ya vipengele hivyo ni: Kwanza, mwalimu anashauriwa kutambua sifa bainifu za wanafunzi wake. Mfano wa sifa hizi bainifu ni pamoja na uwezo wa mwanafunzi wa kusoma, uelewa wao na uwezo wa kutambua ishara za lugha. Pili, mwalimu anahimizwa

kutilia maanani kiwango cha umilisi wa lugha ya wanafunzi. Umilisi wa lugha kulingana na Wanamissouri humwezesha mwanafunzi kuwa na uwezo wa kutumia nyenzo za kufundisha. Tatu, mwalimu anahimizwa kutumia nyenzo ambazo anaweza kumudu gharama yake namwalimu anashauriwa kutumia nyenzo ambazo zinapatikana kwa urahisi; aidha kutoka kwa mazingira ya shule. Iwapo nyenzo husika haipatikani katika mazingira ya shule au nyenzo yenyewe ni ghali mno, mwalimu hanabudi ila kufanya ufaraguzi.

Maoni ya wataalamu hawa kutoka Chuo Kikuu cha Missouri nchini Kolumbia yanalingana na maoni ya  Wright (1989) aliyetaja vipengee vifuvyatavyo vya kuzingatiwa na walimu wanapokuwa wakiteua nyenzo ya kufundishia: kwanza mwalimu anashauriwa achunguze upatikanaji wa nyenzo anayokusudia kutumia. Mwalimu alizidi kushauriwa kuitumia nyenzo ambayo inamvutia mwanafunzi kwa umbo, saizi au rangi. Wright (1989) aliongezea kuwa yafaa mwalimu afikirie kuhusu kiwango cha lugha kitakachotumika wakati wa kuitumia nyenzo hiyo. Kulingana na kauli hii, zoezi litakalotumika kufundisha kipengee fulani cha lugha ya Kiswahili linatakiwa liweze kuzua mazungumzo ya kutosha kati ya wanafunzi kwenye kipindi.

Baada ya mwalimu au mwelekezi kuteua nyenzo mwafaka ya kufundisha, itambidi aitumie vyema. Mifano ya namna za kutumia nyenzo za kufundisha ni pamoja na maonyesho, utandazaji, matumizi ya projekta, utumiaji wa kibinafsi na utumiaji wa pamoja au wa vikundi.

Baada ya mwalimu au mwelekezi kuteua na kutumia njia mwafaka za kutumia nyenzo za kufundisha hana budi kuwa na mazoea kama hayo ili kuinua matokeo ya ufundishaji wake.Kulingana na utafiti uliofanywa na Aduwa na Iyamu (2006) nchini Nigeria katika viwango vya chini na vya juu katika shule za upili kusuhu viwango vya matuimizi ya nyenzo za kufundisha Kiingereza, uligundua kuwa ukosefu wa nyenzo za kufundisha somo la lugha yoyote hausababishi tu matokeo duni katika somo husika bali huathiri hata maendeleo yake katika somo la lugha.Romiszowiski (1988), anatoa sababu moja alipopendekeza vipengele ambavyo huathiri matumizi ya nyenzo za kufundisha. Romiszowiski (1988) aligundua kuwa, ukosefu au upungufu wa nyenzo huathiri matumizi ya nyenzo mahususi ambayo mwalimu angeihitaji. Utaftiulitaka kutathiminikiwango cha mazoea ya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

## 2.4 Athari ya Matumizi ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Kiswahili.

Kwa miaka mingi, nyenzo za kufundisha zimekuwa kiungo muhimu katika kuinua ufundishaji wa lugha yoyote ile.Nyenzo za kufundisha hutumiwa kwa njia nyingi katika mchakato mzima wa kufundisha Kiswahili. Kulingana na maoni ya wataalamu ni wazi kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari nyingi katika ufundishaji wa Kiswahili. Utafiti huu ulibaini athari zifuatazo: Kwanza kabisa vifaa vya kufundisha huwa ni daraja kati ya mwanafunzi na funzo lake. Suleiman (1998) anafafanua kuwa, nyenzo za kufundisha ni zile ambazo huwasilisha ujumbe au habari kutoka kwa mwanzilishi (mwalimu) hadi kwa mpokeaji (mwanafunzi). Suleimani (1998)anadhihirisha kuwa vifaa vya kufundisha huwa kipatanisho kati ya funzo na mawazo ya mwanafunzi.Utafiti ukiegemea maoni ya Suleimani (1998) unasadikisha kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zinapotumika, zinarahisisha ufundishaji na uelewa wa wanafunzi na hivyo kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili na hatimaye kuchangia matokeo bora ya mwanafunzi.

Athari nyingine ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni kuwezesha mihimili ya funzo kusalia kwenye kumbukizi za mwanafunzi kwa muda mrefu. Haya yanafafanuliwa vizuri na msemo kutoka nchi ya Uchina unaonuu kuwa: ‘wakati mtu anapopitishiwa ujumbe kwa njia ya mdomo, kuna uwezekano mkubwa wa ujumbe huo kusahaulika kwa haraka; wakati ujumbe uo huo unapopitishwa kwa msaada wa vifaa, hukumbukika kwa wepesi. Wakati mikono pamoja na matumizi ya nyenzo inapohusishwa, katika harakati za kupitisha ujumbe, uwezo wa binadamu wa ukumbukaji huimarika (Ellis, 1991).Richards (1990) akinukuliwa na Farida (1999) anafafanua kuwa, nyenzo za kufundisha humsaidia mwanafunzi katika ujifunzaji na humwezesha kukumbuka hoja muhimu alizofunzwa. Richards (1990) aliongeza kuwa nyenzo huzidisha shauku, uelewa na ukumbukaji. Haya yanadhibitisha kuwa, nyenzo za kufundisha Kiswahili hutumika katika kukuza uwezo wa wanafunzi wa ukumbukaji. Wanafunzi wanapofunzwa kinadharia, kuna uwezekano wa kusahau kwa haraka kile walichofundishwa. Kwa upande mwingine, wakati nyenzo za ufundishaji zinapohusishwa, uwezo wa ukumbukaji huimarika.

Ili mwanafunzi aweze kuwa madhubuti katika somo la Kiswahili hana budi kuwa na stadi mbalimbali za kumudu somo hili. Stadi hizi ni pamoja na kusoma matini za Kiswahili kwa kaida zifaazo, utungaji wa sentensi, ufahamu wa matini za Kiswahili, uwezo wa kukumbuka na uandishi. Stadi hizi zinahimizwa na Ensaikolopidia ya Nyenzo za Kufundisha (1978) inapoeleza kwamba, nyenzo huongeza shauku, ufahamu na uwezo wa kukumbuka. Maelezo

haya ya Ensaikolopidia huenda yamezua misingi yake kutoka kwa nadharia tete kuwa, ujumbe ukiwasilishwa kidhahania ndivyo utakavyokuwa mgumu kueleweka na kukumbukika.

Stadi hizi za lugha huimarishwa na matumizi ya nyenzo za kufundisha. Kwa mujibu wa Wright (1989) nyenzo za kuonwa hutumika vyema kufundisha usilikilizaji, usomaji, uandishi, uzungumzaji, sarufi na kaida za lugha. Kutokana na maoni ya Ensaikolopidia (1978) na maoni ya Wright (1989), utafiti unasadiki kuwa, stadi kama hizi humpa mwanafunzi wa Kiswahili ujasiri na umilisi wa kuitumia lugha ya Kiswahili na hatimaye kupata matokeo mazuri.

Athari nyingine ya nyenzo za kufundisha ni kuwatia wanafunzi shauku na motisha wakati na baada ya kipindi. Sugiharto (1994) anadai kuwa nyenzo za kufundisha ni vifaa vya kutia motisha na vya kuzua shauku katika ujifunzaji wa lugha. Maoni ya Sugiharto (1994) yanaunga mkono na maoni ya Dale (1999) anayesisitiza kuwa, nyenzo za kufundisha huwa na majukumu mengi katika michakato ya ufundishaji; zaidi huchochea motisha kwenye ujifunzaji. Mbali na kuwa nyenzo humtia mwanafunzi shauku, Sugiharto (1994)anaongeza kuwa, "utumizi wa nyenzo za kufundisha unamwepusha mwalimu na matumizi ya lugha mame wakati wa ufundishaji wa lugha za kigeni".Kutokana na maoni ya wataalamu hawa wawili, utafiti unashauri kuwa ili kuwatia wananfunzi motisha katika somo la Kiswahili, mwalimu hana budi kuzitumia nyenzo za kufundisha. Kwa hivyo, ufundishaji wake wa lugha ya Kiswahili utaimarika na athari zitadhihirika katika matokeo ya mtihani wa kitaifa.

Athari nyingine ya nyenzo za kufundisha ni kule kuchunga muda yaani kutumia muda kikamilifu. Haya yanadhibitishwa na Brown (1993) anayedai kuwa, dhima kuu ya nyenzo za kufundisha ni kuokoa muda, kuchochea shauku na kumpa motisha mwanafunzi kushiriki darasani. Nyenzo hupitisha ujumbe unaokusudiwa kwa muda mfupi. Ili kuokoa muda wakati na baada ya kipindi cha Kiswahili, mwalimu hana budi kutumia nyenzo za kufundisha. Utumizi wa nyenzo za kufundisha Kiswahili unamwezesha mwanafunzi kuwa mshiriki katika kipindi cha Kiswahili. Kushiriki kwa mwanfunzi katika kipindi cha Kiswahili kutachochea shauku na motisha na hivyo kumwathiri mwanafunzi kwa njia bora akilinganishwa na yule ambaye hakutumia nyenzo. Vilevile mwanafunzi akishiriki kikamilifu katika kipindi ataweza kupitia silabasi ya Kiswahili kwa muda ulioratibiwa na wakuza mitaala

Athari nyingine ya nyenzo za kufundisha ni kumwezesha mwanafunzi kuingiliana vyema na tajriba yake. Maoni haya yanathibitishwa na Dales (1999) anaposhauri kuwa, nyenzo za ufundishaji humpa mwanafunzi tajriba yenye mguso na zaidi humwezesha kuingiliana vilivyo na tajriba yake. Nyenzo za kufundisha Kiswahili kama vile matunda hutolewa katika mazingira ya mwanafunzi. Nyenzo kama hizi humfanya mwanafunzi kuhisi kuwa mazingira yake yameletwa darasani na kwa hivyo anakuwa na mwiingiliano mzuri na funzo lake. Kulingana na maoni ya Dales (1999) utafiti unawashauri walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua kutumia nyenzo kutoka katika mazingira ili kuwapa wanafunzi tajriba ifaayo.

Utafiti ulivyozidi kubaini kuwa, nyenzo husimama mahali pa mwalimu. Hivyo basi, mwanafunzi atajifunza akiongozwa na nyenzo husika bila kuwepo kwa msaada mwingi wa mwalimu. Maoni haya yanaungwa mkono na maoni yake Heinrich (1993) anapodai kuwa nyenzo humsaidia mwalimu kuwa mdhibiti bora wa mafunzo ya lugha. Kutokana na maoni yake Heinrich (1993) utafiti unawashauri walimu wa Jimbo la Nyandarua kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili ili wanafunzi waweze kujitegemea katika ujifunzaji. Haya yakizingatiwa, ufundishaji wa Kiswahili utaimarika na hivyo kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika mtihani wa kitaifa.

Athari nyingine ya nyenzo za kufundisha ni kuwa kichocheo kikuu wakati wa kufundisha usomaji wa matini za Kiswahili. Wright (1989) anaeleza kuwa, wakati wa kipindi cha usomaji kuna njia nyingi za kufundisha matini zilizoandikwa. Mwalimu anashauriwa kutumia njia ya mazungumzo, au njia ya picha ili wanafunzi wapate maana kutoka kwa picha hizo. Maelezo ya Wright (1989) yanasadikishwa na Callahan (1992) anapodai kuwa, picha moja inapotumika inafaa kuliko matumizi ya maneno elfu.

Maelezo haya ya kimsingi hutumika katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili. Kwa mfano, ikiwa mwalimu anakusudia kufundisha maana ya neno ‘duma’, picha ya mnyama huyu itaambatanishwa na maelezo ya mdomoni au ya kamusini. Mwalimu atatoa maelezo ya mnyama huyu huku wanafunzi wakitazama picha yenyewe. Zoezi kama hili litazua mwiingiliano wa haraka kati ya mawazo ya mwanafunzi na kile anachofundishwa na hivyo kurahisisha ufundishaji wa somo la Kiswahili. Kulingana na maoni ya Wright (1989) na Callahan (1992), utafiti unawarai walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua kutumia picha katika ufundishaji wa Kiswahili ili kuinua miingiliano ya haraka kati ya funzo na mawazo ya mwanafunzi.

Dhima kuu ya nyenzo ya kufundisha ni kusadia maingiliano ya kimafunzo kati ya mwalimu na mwanfunzi (Latuheru, 1988). Maoni ya Latuheru (1988) yanahimiza kuwepo kwa uwili wa mawasiliano wakati wa ufundishaji kati ya mwalimu na mwanafunzi au baina ya wanafunzi wenyewe. Dales (1999) aligawa dhima kuu ya nyenzo za kufundisha katika pandembili. Dhima kuu ya kwanzanikule kusaidia katika utoaji wa mafunzo. Nayo dhima kuu ya pili ya nyenzo ni kusaidia ujifunzaji. Nyenzo za utoaji wa mafunzo kulingana na Dales (1999), ni zile zinazotumiwa na mwalimu anapokuwa akifundisha. Nazo nyenzo za ujifunzaji ni zile zinazotumiwa na wanafunzi wenyewe wakati wa ujifunzaji wao. Dales (1999) anazidi kuongeza kuwa nyenzo za kufundisha humsaidia mwalimu na welekezi wengine kudhibiti mafunzo vilivyo. Kulingana na maoni ya Latuheru (1988) na Dales (1999), utafiti unawahimiza walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua kutumia nyenzo za kufundisha ili kuimarisha mawasiliano darasani baina yao na wanafunzi wao. Mawasiliano yakiimarika yatachangia matokeo mema ya somo la Kiswahili katika mtihani wa kitaifa.

Somo la Kiswahilikatika shule za msingi nchini, linaweza kufanywa kuwa la kuvutia zaidi kupitia kwa matumizi ya nyenzo za kufundisha. Tukiazima maoni ya Okwako (1994) kuhusu uimarishaji wa uandishi wa insha ya Kiingereza, anadai kuwa 'Wakati wa kipindi cha uandishi, projekta, mabango ya sumaku na hata kompyuta zinamsaidia mwalimu kuonyesha athari za kuongeza, kutoa au kufanyia mabadiliko herufi ili kufaa uandishi wa insha ya Kiingereza'.Vivyo hivyo, mwalimu wa Kiswahili anaweza kutumia nyenzo wakati wa kufundishia insha ya Kiswahili, sarufi na vipengee vingine vya lugha ili kuweza kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili. Maoni haya ya Okwako (1994) yanathibitishwa na Mbuthia (1996) aliyefanya utafiti kuhusu ulinganisho wa njia mbili za kufundisha uandishi wa Insha katika somo la Kiswahili katika Manispaa ya Eldoret. Njia moja ilihusu utoaji wa mafunzo pamoja na usaidizi wa nyenzo, nayo njia ya pili ilihusu ufundishaji wa insha ya Kiswahili bila matumizi ya nyenzo za kufundisha. Utafiti ulibaini kuwa, matokeo ya ufundishaji wa somo la uandishi katika mizani ya Likert ni wa kuridhisha wakati ambapo nyenzo za kufundisha zinapotumiwa ikilinganishwa na matumizi ya njia za kimapokezi kama ya maongezi. Kupitia kwa utafiti huo ilibainika kuwa walimu wengi hawatumii nyenzo zozote wakati wa ufundishaji wa somo la Kiswahili. Kulingana na maoni ya wataalamu hawa wawili, Okwako (1994) na Mbuthia (1996), ni wazi kuwa nyenzo huchangia katika matokeo ya mwanafunzi katika somo la Kiswahili.

Majukumu na athari za nyenzo za kufundisha Kiswahili hayawezi yakapuuzwa. Hivyo basi, uangalifu wakati wa mutumizi ya nyenzo hizi ni sharti uwepo. Matumizi ya nyenzo yanakusudiwa kuwa na matokeo chanya katika ufundishaji wa Kiswahili. Maoni haya yanathibitishwa na matokeo ya utafiti uliofanywa na Aduwa na Iyamu (2006) nchini Nigeria. Wataalamu hawa waligundua kuwa iwapo walimu wa shule za umma za sekondari za daraja la chini na la juu nchini Nigeria wangekubali kugeukia matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiingereza na teknolojia yake wangevumbua mbinu mpya za ufundishaji kuliko kutegemea vitabu vya kozi, ubao na mbinu ya mhadhara. Tukiegemea maoni ya watafiti hawa na kulinganisha mbinu za ufundishaji wa Kiingereza na zile za Kiswahili, utafiti unaonyesha kuwa, matumizi sawia ya nyenzo za kufundisha Kiswahili yatamwepushia mwalimu mbinu za kimapokezi za ufundishaji na kumwalika katika uwanja wa matumizi ya mbinu za kisasa za kufundisha Kiswahili. Mbinu hizi mpya zinajumulisha matumizi ya nyenzo wakati na baada ya kufundisha Kiswahili; hivyo basi kuathiri ufundishaji wa somo la Kiswahili. Matokeo yake yanadhihirika katika utendaji wa mwanafunzi katika somo hili la Kiswahili

Kulingana na utafiti huu, athari na majukumu ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni anuwai. Majukumu na athari hizi za nyenzo yanajumulishwa na Richards akinukuliwa na Sugiharto (1994)kama: Dhima ya kumakinika, dhima ya mawasiliano na dhima ya funzo kubaki kwenye mawazo kwa muda mrefu. Dhima kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza iwapo nyenzo za kufundisha Kiswahili zinatosheleza majukumu haya matatu katika Jimbo la Nyandarua.

### 2.5. Changamoto Za Matumizi ya Nyenzo za KufundishaKiswahili

Walimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua hukabiliwa na changamoto nyingi wakati wa kuteua na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili.

Walimu wa Jimbo la Nyandarua waliainisha changamoto nyingi zinazowakabili katika matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Changamoto hizi kwa kiasi kikubwa huchangia upungufu au upatikanaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua. Utafiti huuulichunguza iwapo walimu wa Jimbo la Nyandarua wanakabiliwa na changamoto zozote wakati wa utumiaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili. Vilevile, utafiti ulichunguza iwapo walimu hawa wamechukua hatua zozote za kukabiliana na changamoto hizi.

Utafiti uligundua kuwa mojawapo wa changamoto inayowakabili walimu wa Jimbo la Nyandarua ni ukosefu wa fedha za kununua nyenzo za kufundisha Kiswahili. Changamoto hii inalingana na mapendekezo ya Strauss na Frost (1999) kuhusu vipengele muhimu vya kuzingatiwa na walimu wakati wa kuteua nyenzo za kufundisha. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni uwezo wa taasisi wa kumudu gharama ya nyenzo fulani. Taasisi inaweza kushindwa kugharamia nyenzo ambayo mwalimu wa Kiswahili huenda akaihitaji. Jambo kama hili huenda likamvunjamoyo mwalimuna ufundishaji wa somo la Kiswahili ukaathirika. Maoni haya ya Strauss na Frost (1999), yanaungwa mkono na mapendekezo ya Chuo Kikuu cha Missouri Nchini Kolumbia (2012) kuhusu vipengele kumi na vitatu vya kuzingatiwa na walimu wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni gharama ya nyenzo husika.

Kipengele kingine kilichopendekezwa na Wanamissouri ni kuhusu ukosefu wa wakati wa kutayarisha nyenzo za kufundisha. Utafiti huu pia ulibaini kipengee cha wakati kuwa kikwazo kikubwa kwa walimu wa Jimbo la Nyandarua wanaofundisha Kiswahili.

Changamoto nyingine katika matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahilini kuteua nyenzo zinazohitilafiana na shabaha ya funzo. Changamoto hii inafafanuliwa zaidi na Chuo Kikuu cha St Cloud (2009), nchini Marekani, kilipopendekeza hatua zinazofaa kuzingatiwa na walimu wakati wa kuteua nyenzo za kufundisha. Miongoni mwa hatua hizi ni kuwa mwalimu huhitajika kuteua nyenzo kulingana na shabaha anayokusudia. Ili kuteua nyenzo inayostahili, mwalimu hana budi kufanya maandalizi kwa utendeti. Maandalizi ya aina hii huchukua muda mwingi kama anavyoshauri Lewis (1985), anaposisitiza kuwa mwalimu anatakiwa kufanya maandalizi kwa utendeti. Kutokana na mashauri ya chuo kikuu cha St Cloud na ushauri wa

Lewis (1985) utafiti unamshauri mwalimu wa Kiswahili kujiandaa na kutayarisha nyenzo yake barabara kabla ya kuingia darasani.

Changamoto nyingine ambayo inawakabili walimu wa Kiswahili katika matumizi ya nyenzo za kufundisha ni ukosefu wa tajriba ya kutosha ya kutayarisha na kuteua nyenzo. Chuo Kikuu cha Missouri (2012) nchini Kolumbia kinatoa rai kuwa,mwalimu asiye na tajriba ya kutosha hushindwa kutumia nyenzo yoyote wakati wa ufundishaji wake.

Mitazamo hasi ya walimu dhidi ya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni changamoto nyingine ambayo utafiti uligundua. Mwalimu anaweza kuwa na mitazamo hii hasi kwa sababu nyingi. Romiszowiski (1988) anatoa sababu moja alipopendekeza vipengele ambavyo huathiri matumizi yanyenzo za kufundisha. Aligundua kuwa, ukosefu au upungufu wa nyenzo huathiri matumizi ya nyenzo mahususi ambayo mwalimu angeihitaji. Upungufu huu humvunja moyo na kumfanya kuwa na mtazamo hasi kuhusu utumiaji wa nyenzo za kufundisha.

Changamoto zinazowakabili walimu wanapokuwa wakiteua na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili ni nyingi. Utafiti huu ulichunguza ni kwa kiwango kipi changamoto hizi zinaathiri ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

## 2.6. Nadharia ya Utafiti

Utafiti ulijikita kwenye nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo. Waasisi wa nadharia hii ni Daft na Lengel (1986). Wataalamu hawa waliegemea nadharia ya Mikakati ya Mawasiliano*(information processing theory*) ili kukuza mihimili yake. Nadharia hii ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo ilianzishwa kuelezea na kutathmini nyenzo za mawasiliano katika mashirika mbalimbali ya kibiashara. Daft na Lengel (1986) walikusudia kusaidia mashirika ya kibiashara kukabiliana na changamoto za mawasiliano kama vile ujumbe usioeleweka yaani wenye utata au ujumbe ukaokanganya. Nadharia hii imefanyiwa majaribio zaidi ili kuweza kiimarishwa. Hivi karibuni nadharia ya uwezo wa Matumizi ya Nyenzo imejumlisha nyenzo za kisasa za mawasiliano kama vile mikutano ya mitandaoni. Hata ingawa nadharia hii inajihusisha zaidi na matumizi ya nyenzo kuliko uteuzi wa nyenzo, utafiti zaidi unafichua kuwa inahusika na njia ya kupitisha ujumbe. Tangu kuasisiwa kwa nadharia hii ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo, imetumika katika nyanja mbalimbali zikiwemo za kielimu.

Daft na Lengel (1986) walieleza 'ukwasi wa ujumbe' kuwa ule uwezo wa ujumbe kubadili uelewa kadri muda unavyozidi kubadilika. Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo humsaidia mtumiaji kuwasiliana kulingana na mabadiliko ya uelewa wa ujumbe. Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo hupima nyenzo za mawasiliano kulingana na uwezo wa nyenzo husika wa kuwasilisha ujumbe ulio changamano. Ikiwa nyenzo inatumika kuelezea jumbe tofutitofauti pamoja na kuondoa utata wa uelewa basi nyenzo hiyo ni ya kiwango cha juu. Kwa upande mwingine, nyenzo ya kiwango cha chini ni ile ambayo inachukua muda kuwasilisha ujumbe unaotarajiwa

Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo inaeleza kuwa nyenzo zote za mawasiliano huwa na sifa bia ambazo huzifanya kuwa au kutokuwa na uwezo ufaao wa kuwasilisha ujumbe. Daft na Lengel (1986) wanaelezea kuwa, madhumuni makuu ya kutumia nyenzo ni kuondoa utata wa uelewa wa ujumbe. Daft na Lengel (1986) waliihuzisha nadharia hii na ule uwezo wa ujumbe kubadilisha uelewa wa ujumbe kadiri wakati unavyozidi kubadilika. Walibaini kuwa ikiwa ujumbe una utata wa uelewa basi inabidi nyenzo faafu zaidi itumika ili kuwasilisha ujumbe.

Msukumo wa uwezo wa nyenzo wa kuondoa utata wa uelewa wa ujumbe pamoja na kuondoa fafanuzi sizizofaa ndilo jambo la kimsingi wakati wa uteuzi wa nyenzo. Nyenzo yenye uwezo wa hali ya juu inahitajika iwapo ujumbe fulani haueleweki kwa urahisi. Nyenzo yenye uwezo wa kiwango cha chini inafaa wakati ambapo ujumbe unaowasilishwa ni sahili kwa mpokeaji.Mafunzo mengine huhitaji nyenzo ambazo zina uwezo wa hali ya juu wa kuwasilisha ujumbe. Kwa mfano, wakati wa kufundisha somo la matamshi, programu ya mwalimu wa redio huwa kamilifu zaidi kuliko matumizi ya chati za kuchorwa kwa mikono. Mwalimu huyu wa redio hutamka maneno na yakaigwa na wanafunzi wanaomsikiliza. Video kwa upande wake inafaa kuliko kipindi cha redio kwani mwanafunzi hutazama na husikiliza maneno yakitamkwa. Video huonyesha ishara za usoni pamoja na mikao ya midomo wakati wa utamkaji wa maneno. Vilevile, miondoko ya mwili itadhihirika na kufahamika bayana. Hivyo basi, video ina njia nyingi na zenye athari kuu ya kuwasilishia ujumbe unaohitajika kuliko chati au redio. Hivyo basi, mwalimu wa Kiswahili hushauriwa kutumia nyenzo ambayo itaweza kupitisha ujumbe kwa urahisi na kwa ukamilifu ufaao.

Utafiti zaidi wa nadharia hii uliofanywa ulijumulisha vipengele vya kuzingatiwa wakati wa utumiaji wa nyenzo za kuwasilishia ujumbe wowote ule kwa hadhira yoyote ile. Kwa mfano,

ili mwalimu ateue nyenzo ya kufundisha Kiswahili ni lazima azingatie upatikanaji wake; aidha kutoka kwa mazingira ya shuleni au mazingira ya nyumbani. Nyenzo za kufundisha hupatikana kwa njia nyingi. Baadhi ya njia hizi ni kufaragua, kununuliwa, kutengenezwa au upatikanaji wa kifaa halisi. Iwapo nyenzo itanunuliwa ni vyema kujua kama taasisi husika itamudu gharama yake.

Nadharia hii ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo ina mizani ambayo hupima hali ya utata wa ujumbe. Kiwango cha chini cha utata wa ujumbe hudhihirisha kuwa ujumbe ulieleweka na iwapo kiwango cha utata ni cha hali ya juu katika mizani hii, basi ujumbe haukueleweka vilivyo. Hivyo basi, nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo ilitumika kuorodhesha na kutathimini ubora wa baadhi ya nyenzo za kuwasilisha ujumbe zikiwemo simu tamba, barua pepe na ufundishaji kupitia kwa video. Nadharia hii ilitumika kama mizani ya kupima uwezo na utumikaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo inaudhaifu wake. Watafiti wengi wameisuta kuwa inalenga tu uwezo wa nyenzo husuka na kupuuza mambo mengine yanayoathiri matumizi ya nyenzo. Markus (1994) anahoji kuwa misukumo ya kijamii inaathiri matumizi ya nyenzo kuliko tu uwezo wa nyenzo husika. Markus (1994) anazidi kuhoji kuwa nyenzo ambayo inaonekana kuwa hafifu inaweza kuwasilisha ujumbe kuliko ili ambayo inaonekana kuwa ya kiwango cha juu. Utafiti ukiegemea maoni ya Markus (1994) unatoa mfano wa hali kama hii. Kadi ya maneno huwasilisha ujumbe kikamilifu kuliko programu za tarakilishi.

Nao Ngwenyama, Ojelanki & Allen(2006) wanaikosoa Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo kwa kudai kuwa haitilii maanani mila na desturi za mtumiaji. El – Shinnaway& Lyne (2009) wanaikosoa nadharia hii kwa kudai kuwa haikidhi mahitaji ya teknolojia ya kisasa ambayo yanajumlisha nyenzo kama mitandao, baruapepe na mazungumzo ya mitandaoni.

Ili kudhibiti udhaifu wa Nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo, waalamu wameimarisha nadharia hii kwa kubuni nadharia kadhaa. Kock (2005) anaikosoa nadharia hii kwa kusema kuwa baadhi ya nadharia teteza nadharia hii zinaukosefu wa misingi ya kisayansi. Kock (2005)alipendekeza nadharia mbadala ya Uhalisia wa Nyenzo (*media Naturalness Theory).* Kock (2005) alizizua viambajengo vya nadharia hii kutoka kwa mihimili ya Nadharia ya Mageuko ya Binadamu. Kock (2005) anapendekeza kuwa nyenzo


yoyote ambayo inatumiwa ni sharti iwasilishe ujumbe jinsi ujumbe huo ungewasilishwa kupitia kwa njia ya uso kwa uso.

Imedhihirika kupitia kwa tafiti nyingi kuwa walimu wengi hawatumii nyenzo wakati wa kutoa mafunzo yao katika masomo mbalimbali likiwemo la Kiswahili hapa nchini Kenya. Kutokana na hali hii matokeo ya mitihani ya kitaifa ya wanafunzi huwa duni. Ili kuepuka hali hii,nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo huwa mizani bora ya kupima utendakazi wa nyenzo katika ufunzaji wa Kiswahili. Kutokana na jukumu hili kuu ndipo nadharia ya Uwezo wa Matumizi ya Nyenzo iliteuliwa kutathimini ufaafu wa nyenzo ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya

## 2.7. Mgofu Dhanifu

Kutokana na nadharia ya utafiti, mtafiti aliibuka na mgofu dhanifu ufuatao:

Mchoro 2.1 Mgofu Dhanifu wa Utafiti




Kutokana na mgofu dhanifu huu, kibadiliki huru cha utafiti huu ni matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili. Kuna njia tofauti za kutumia nyenzo wakati wa ufunzaji wa Kiswahili. Njia mojawapo ni kutumia nyenzo kimakundi. Njia nyingine ni ya kutumianyenzo kibnafsi yaani mwanafunzi akiwa pekee yake.Kibadiliki hiki huru huathiriwa au hukosa kuathiriwa na kibadiliki cha kati. Kibadiliki cha kati cha utafiti huu kinahusisha mazingira na hali za wanafunzi. Mazingira ya mwanafunzi yanaweza kuwa au kutokuwa na nyenzo ambazo zinahusiana na uimarishaji wa ufundishaji wa somo la Kiswahili. Hivyo basi, mwanafunzi huathiriwa kwa njia moja au nyingine. Kibadiliki cha kati huwa na athari chanya au hasi ambazo zinadhihirika katikakibadiliki tegemezi. Kibadiliki tegemezi cha utafiti huu ni athari ya matumizi ya nyenzo za ufundishaji wa Kiswahili. Athari hizi hudhihirika katika viwango tofauti. Baadhi ya viwango hivi ni kuwa, mwanafunzi huwasiliana kwa ufasaha na kuimarisha utendaji wake wa jumla katika somo la Kiswahili. Iwapo kibadiliki cha kati kingepuuzwa, matokeo ya athari ya matumizi ya nyenzo za ufundishaji katika Kiswahili yangedhihirika moja kwa moja kama uimarishaji wa ufundishaji wa Kiswahili.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1. Utangulizi

Sura hii inashughulikia njia za utafiti zilizotumika. Njia hizi ni; muundo wa utafiti, eneo la utafiti, mbinu za utafiti, idadi lengwa ya utafiti, jumla ya idadi ya sampuli na taratibu za kupata sampuli, uundaji wa vifaa vya utafiti na jinsi ambavyo vifaa hivyo vilivyotolewa kwa watafitiwa. Kisha, sura ilionyesha njia za kuwasilisha data na jinsi ya kuichanganua.

## 3.2. Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumika katika utafiti huu ni wa kimaelezo. Kulingana na Kothari (2004) muundo huu unahusu taratibu za kukusanya data kwa minajili ya kujibu maswali yanayohusiana na hali ya mambo. Muundo huu uliteuliwa kwa sababu unafaa kwa uchunguzi wa kina. Vilevile, unamwezesha mtafiti kukusanya data kwa wakati maalum na kuitumia kueleza hali halisi ya mambo jinsi yalivyo (Cohen, Mnion na Morrizon, 2000). Data inayokusanywa huonyesha hali ya mambo na taratibu zinazochipuka kwa wakati huo, kutambulisha mahusiano na kubainisha mahitaji na mabadiliko yake. Muundo huu wa kimaelezo ulisaidia kukusanya data ili kuelezea hali halisi kuhusu matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

Muundo huu wa kimaelezo, ulifaa katika kuelezea aina za nyenzo za kufundisha Kiswahili, kutathmini kiwango cha matumizi ya nyenzo na changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.Muundo huu ulisaidia kutoa suluhuza changamoto hizo.

## 3.3. Eneo la Utafiti

Jimbo la Nyandarua linapatikana katika sehemu ya katikati ya nchi, ambayo ilijulikana zamani kama mkoa wa kati. Jimbo hili linapakana na Jimbo la Laikipia kwa upande wa Kaskazini na Kaskazini Mashariki, majimbo ya Nyeri na Murang’a kwa upande wa Mashariki, Jimbo la Kiambu kwa upande wa Kusini na Jimbo la Nakuru pande za Kusini Magharibi na Magharibi. Jimbo la Nyandarua limegawika katika vijimbo saba. Vijimbo hivi ni Nyandarua Kaskazini, Nyandarua Magharibi, Mirangi-ini, Kipipiri, Nyandarua Kusini, Nyandarua Kati na Kinangop.

Tafiti zilizofanywa katika maeneo mengine nchini Kenya kama Jimbo la Bungoma zimedhihirisha kuwa shule nyingi za msingi nchini Kenya zinakabiliwa na tatizo la matumizi ya nyenzo za kufundisha. Ukosefu huu umeathiri uimarishaji wa ufundishaji katika masomo mbalimbali. Imedhihirika kuwa hakuna utafiti wa hivi karibuni ambao ulikuwa umefanywa katika Jimbo la Nyandarua kuhusiana na nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma. Kufuatia uegemeaji wa misingi hii ndipo Jimbo la Nyandarua liliteuliwa kama eneo la utafiti huu. Utafiti huu ulinuia kuchunguza matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya.

### 3.4. Sampuli lengwa

Jimbo hili lina jumla ya shule za msingi za umma mia tatu na thelathini na moja. Walimu katika sampuli lengwa ni 369 ambao hufundisha Kiswahili katika darasa la nane. Walimu hawa walishirikishwa kwa sababu wao ndio watekelezaji wa silabasi ya Kiswahili katika darasa hili la nane. Isitoshe, walimu wawa hawa ndio wateuzi na waelekezi wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Walimu wakuu walioshirikishwa ni 331. Walimu wakuu ndio wafadhili wakuu wa nyenzo zote za ufundishaji katika shule za msingi za umma. Walimu wakuu wamepewa jukumu la kununua na kupanga mikakati ya upatikanaji wa nyenzo za kufundisha zikiwemo za Kiswahili. Kwa jumla idadi ya sampuli lengwa ni walimu 700; yaani walimu 369 wanafundisha Kiswahili katika darasa la nane na walimu wakuu 331.

### 3.5.Uteuzi wa Sampuli Kamili ya Utafiti

Kiwango katika sampuli kamili hutegemea vigezo vya idadi lengwa ya utafiti na makisio anayokusudia mtafiti (Cooper, 1998). Mtaalamu Gay (1983) anapendekeza kuwa angalau asilimia 10% ya sampuli lengwa iteuliwe kama sampuli kamili. Kulingana na maoni ya Cooper (1998) na maoni ya Gay (1983), utafiti huu ulitumia angalau asilimia 10% ya walimu wakuu na walimu wanaofundisha Kiswahili kutoka katika kila kijimbo kama sampuli kamili.

Vijimbo vyote saba vya Jimbo la Nyandarua vilihusishwa katika utafiti huu. Mbinu ya uteuzi wa sampuli kimakusudi ilitumika kuteua sampuli ya walimu wakuu kutoka kwa kila kijimbo.Utafiti ulitumia vijimbo hivi saba kulingana na mipaka ya kiutawala. Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza mbinu ya uteuzi wa sampuli kimakusudi kama mbinu ambayo inamwezesha mtatifi kuchukua data kutoka kwa watafitiwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Matokeo ya mbinu hii ni kuwa kila sehemu ya eneo la utafiti iliwakilishwa.

Mbinu ya unasibu ilitumika kuteua idadi ya shule katika kila kijimbo. Ili kupata ni shule gani hasa ambayo ingewakilisha kijimbo bila mapendeleo, mtafiti aliandika majina ya shule zote katikakijimbo husika kwenye vijikaratasi vidogo, kisha vijikaratasi hivyo vikaingizwa katika debe moja. Baadaye mtafitialiteua sampuli kamili kinasibu kulingana na idadi iliyotakikana ya kijimbo. Mtafiti alirudia hatua hizi katika kila kijimbo. Baadaye mtafiti alijumlisha idadi ya shule katika kila kijimbo na kupata sampuli kamili ya shule 46. Hii ni asilimia 13.9% ya idadi lengwa. Walimu wakuu wa shule hizi ndio walioteuliwa kama watafitiwa wa hojaji ya walimu wakuu. Mbinu ya unasibu ilitumika kwa sababu kila shule ilitarajiwa kupata nafasi sawa ya kuhusishwa bila mapendeleo. Kombo na Tromp (2006) walifafanua kuwa mbinu hii humwezesha mtafiti kuteua wahusika ambao anaamini kuwa watampa data anayohitaji.

Ili kupata sampuli ya walimu 55wanaofundisha Kiswahili katikadarasa la nane, mtafiti alirudia hatua alizotumia kuteua sampuli ya walimu wakuu. Sampuli ya walimu 55 ni asilimia 14.91% ya idadi lengwa ya walimu wote wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane katika Jimbo la Nyandarua. Matokeo haya ya uteuzi wa sampuli yanaonyeshwa katika jedwali 2 lifuatalo:

**Jedwali 2: Uteuzi wa Sampuli ya Utafiti**

| Kijimbo | Sampuli lengwa | | Sampuli kamili | | % | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Walimu wa Kiswahili | Walimu wakuu | Walimu wa Kiswahili | Walimu wakuu | Walimu wa Kiswahili | Walimu wakuu |
| **Nyandarua Kaskazini** | 75 | 68 | 11 | 9 | 14.67% | 13.76% |
| **Mirangiini** | 35 | 30 | 6 | 5 | 17.17% | 16.67% |
| **Nyandarua Magharibi** | 45 | 42 | 7 | 6 | 15.56% | 14.28% |
| **Nyandarua Kati** | 44 | 41 | 7 | 6 | 17.07% | 14.63% |
| **Kipipiri** | 70 | 64 | 10 | 8 | 14.28% | 12.50% |
| **Nyandarua Kusini** | 50 | 45 | 7 | 6 | 14.00% | 13.33% |
| **Kinangop** | 50 | 41 | 7 | 6 | 14.00% | 14.63% |
| **Jumla** | 369 | 331 | 55 | 46 | 14.91% | 13.90% |

### 3.6 Vifaa vya Utafiti

Ili kupata matokeo yaliyokusudiwa kuhusu matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua,utafiti ulitumia hojaji mbili. Kulingana na Gay (1983) hojaji humpa mtafitiwa uhuru wa kutoa maoni na mapendekezo yake kuhusu jambo fulani. Ni kwa misingi hii basi ndipo hojaji iliteuliwa kama kifaa kikuu cha kukusanya data.

#### 3.6.1 Hojaji

Katika utafiti huu hojaji mbili zilitumika. Hojaji moja ilijazwa na walimu wakuu na ya pili ilijazwa na walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane.

Hojaji ya walimu wakuu ilishughulikia maswali kuhusu upatikanaji wa nyenzo za kufundisha kwa jumla. Yamkini, walimu wakuu ndio wana jukumu la kuhakikisha kuwanyenzo zakufundisha zinapatikana, kwani ndio wafadhili wakuu. Walimu wakuu

wanalojukumulingine lakuhakikisha kuwa mitaala inafuatwa shuleni. Mitaala huhusishamatumizi ya nyenzo zakufundisha.

Utafiti unasadiki kuwa walimu wengi wakuu hawafundishi somo la Kiswahili na kwa hivyo hojaji hii ilitumia lugha ya Kiingereza. Maswali saba ya hojaji hii ni funge ilhali swali moja ni huru. Maswali funge ya hojaji ya walimu wakuu yalihusu usuli wa watafitiwa, aina za nyenzo za kufundisha Kiswahili, viwango vya matumizi yanyenzo za kufundisha Kiswahili, athari ya nyenzo za kufundisha Kiswahili na changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Nalo swali funge lilihusu jinsi ya kuimarisha matumizi ya nyenzo za Kiswahili katika shuleza msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua. Kwa jumla maswali yote katika hojaji hii ya walimu wakuu yalikuwa ni manane.

Madhumuni makuu yahojaji ya walimu wanaofundisha Kiswahili yalikuwa kuhusu matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili na athari ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.Maswali haya yaliambatana na madhumuni ya utafiti. Hojaji hii ina maswali kumi na moja. Maswali haya yalihusu; usuli wa watafitiwa, aina za nyenzo za kufundisha Kiswahili, viwango vya matumizi ya nyenzo, athari ya nyenzo za kufundisha na changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.

Walimu wanaofundisha Kiswahili ndio watekelezi wa silabasi ya darasa la nane. Silabasi humwongoza mwalimu wakati wa kuteua na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili. Kwa jumla maswali yote ya hojaji yalikuwa kumi na tisa.

### 3.7. Uthabiti na Uhalali wa Vifaa vya Utafiti

Uthabiti na uhalali wa vifaa hudhihirika ikiwa kifaa chenyewe kinachunguza na kuwa na matokeo ya kuridhisha kulingana na kiwango kinachohitajika (Borg na Gall, 1996). Ili kupata uthabiti na uhalali wa vifaa vya utafiti, miitiko kutoka kwa utafiti wa majaribio ilichanganuliwa na ilitumika kupigia msasa maswali ya hojaji. Mtafiti kupitia kwa msaada wa wasimamizi walioteuliwa na chuo hiki alifanya marekebisho katika hojaji.

### 3.8. Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti

Kwa mujibu wa Joppa (2000), ikiwa kifaa chochote kinaweza kutoa matokeo yanayofanana baada ya kujaribiwa kwa mara kadhaa, basi kifaa hicho ni cha kutegemewa.Vifaa vya utafiti huu vilitumiwa tena baada ya majuma mawili kwenye shule zizo hizo ambazo zilifanyiwa majaribio. Ili kupima uaminifu wa vifaa hivi, mbinu ya majaribio ilitumika. Mbinu hii

inahusisha kutoa hojaji mara mbili kwa kundi moja kwa kipindi cha wiki mbili. Matokeo ya majaribio haya mawili hulinganishwa. Kisha, kigezi uwiano cha Pearson kilitumika kupimia uhusiano wa seti hizi mbili za data. Kigezi cha Pearson hutumia fomula ifuatayo;

$$r = \frac{Exy}{\sqrt{Ex^2y^2}}$$

Ikiwa kigezi hiki ni kati ya 0.6 hadi 1, basi vifaa vya utafiti ni vya kuaminika. Baada ya kufanyiwamajaribio na kupimwa kwa kutumia kigezi cha uwiano cha Pearson, matokeo yalikuwa 0.75. Matokeo haya basi yanaonyesha kuwa vifaa hivi ni vya kutegemewa katika utafiti huu.

### 3.9. Majaribio ya Vifaa

Vifaa vya utafiti hufanyiwa majaribio ili kuhakikisha kuwa vina uwezo wa kukusanya data inayohitajika (Mugenda na Mugenda, 1999). Hojaji za utafiti huu zilifanyiwa majaribio katika shule tano za msingi zaumma katikaJimbo la Nyandarua. Mbinuya uteuzi wa sampuli kimakusudi ilitumika kuteua vijimbo vitano vya Jimbo la Nyandarua. Mbinu ya unasibu ilitumika kuteua sampuli za walimu wakuu na walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane kwenye maeneo haya matano.Baadaya wiki mbili, utaratibu huu ulirudiwa katika shule zizo hizo tano. Matokeo yake yalichanganuliwa ili kuhakikisha ufaafu wa vifaa hivi. Maswali yaliyokuwa na dosari yalisahihishwa. Matokeo ya majaribio haya yalimwezesha mtafiti kukisia kiwango chamiitiko ya watafitiwa. Shule zilizofanyiwa utafiti wa majaribio hazikushirikishwa katika utafiti wenyewe.

### 3.10. Ukusanyaji wa Data

Idhini ya kufanya utafiti katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua ilitolewa na Wizara ya Elimu. Baada ya idhini kutolewa, mtafiti alitembelea shule zilizoteuliwa kama sampuli kamili na kuwafahamisha walimu wakuu kusudi lake. Kupitia kwa walimu wakuu, mtafiti aliomba usaidizi aliokusudia.

Hojaji zilipokezwa walimu wakuu na walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane. Mtafiti aliwafahamisha kwa muhtasari lengo la utafiti wenyewe, pamoja na kusudi la utafiti. Mtafiti alichukua miitiko baadaye kulingana na maafikiano na watafitiwa.

Baada ya watafitiwa kukabidhiwa vifaa vya utafiti, walipewa muda wa kutosha wa kufahamu shabaha yazo ili kutoa miitiko iliyotarajiwa. Mtafitiwa alifahamishwa kwa kina yaliyomo kwenye vifaa hivi ili aweze kutoa miitiko iliyotarajiwa.

### 3.11. Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulianza punde tu baada ya mtafiti kukusanya hojaji. Katika hatua hii data kutoka kwa vifaa hivi ilihaririwa, ikasimbwa na kuingizwa katika mfumo wa SPSS. Mtafiti aliziharir vifaa vya utafiti ili kujaribu kuondoa makosa na dosari. Miitiko yote iliwekwa katika kategoria zilizotakikana. Mtafiti aliisimba data kutoka kwa vifaa vya utafiti kwa kuwekwa nambari kwenye majibu. Kila kategoria ilifuata madhumuni ya utafiti huu.

Ili kuhakikisha upatikanaji wa data moja kwa moja kutoka kwa hojaji, mtafiti aliyasimba maswali funge kwa kuweka nambari ya siri katika kila swali husika. Miitiko kutoka kwa maswali funge iliwekwa katika kategoria chache kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Miongoni mwa maswali funge kulikuwa na swali la kalibu. Swali hii lilimtaka mtafitiwa kuteua miitiko kutoka katika mizani ya Likert. Katika mizani hii nambari ziliambatanishwa na majibu kulingana na ukubalifu wa athari za nyenzo katika ufunzaji wa Kiswahili. Kwa mfano, katika swali la 9b kwenye hojaji ya walimu wanaofundisha Kiswahili, mtafitiwa aliteua miitiko kuhusu athari za nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili kutoka katika safu ya majibu aliyopewa. Miitiko kutoka kwa swali hili ilisimbwa kulingana na ukubalifu wa mtafitiwa kuhusu athari ya nyenzo. Kwa mfano nambari 1 iliashiria kuwa, mtafitiwa anakubali kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zinamwathiri mwanafunzi katika ufundishwaji wake wa somo la Kiswahili, nayo nambari 5 iliashiria hali ya kutokubali kuwa nyenzo za kufundisha zina athari yoyote. Misimbo hii vilevile ilizua kategoria 5 ambazo zilichangia kuwepo au kutokuwepo kwa athari ya nyenzo katika ufunzaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua.

Maswali wazi ya hojaji yalichambuliwa kupitia kwa kwa mfumo wa uchanganuzi wa maudhui. Miitiko ya maswali iliteuliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Baadaye miitiko ilirekodiwa na kusimbwa na kuwekwa kwa kategoria zilizotakikana.

Baada ya data kusimbwa, ilitiwa kwenye mfumo wa SPSS ili ichanganuliwe. Mtafiti aliandaa ripoti huku akionyesha uhusiano baina ya misimbo na mada zilizokuwa zikichanganuliwa. Mtafiti aliandaa muhtasari wa matokeo kama yalivyojitokeza kwenye utafiti. Baada ya kulinganua, mtafiti alitambua ruwaza na mitindo ya matokeo ya uchanganuzi. Hii ilifanywa

kwa njia ya maelezo ambapo majedwali, grafu na asilimia ndizo zilizotumika kuelezea matokeo ya utafiti.

### 3.12 Maadili ya Utafiti

Trochim (2002) alipendekeza kuwa utafiti unafaa kufuata maadili kama kuomba ruhusa ya kuwashirikisha watafitiwa. Mtafiti aliandaa kikao na watafitiwa na kuwajulisha kusudi lake.Baadaye, mtafiti aliwaelezea watafitiwa azma yake kuu, pamoja na kuwaomba idhini ya kuwashirikisha. Kisha aliwahakikishia kuwa miitiko yao ingetumika kwa madhumuni ya utafiti huu tu na wala sio kwa kusudi lingine lolote.

# SURA YA NNE

## Uchanganuzi wa Data na Majadiliano ya Matokeo ya Utafiti

### 4.1Utangulizi

Sura hii inashughulikia uwasilishaji, uchanganuzi wa data na majadiliano ya matokeo ya utafiti. Sehemu hii inaongozwa na madhumuni ya utafiti ambayo ni: Kuainisha nyenzo zinazotumika na walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kenya, Kutathimini kiwango cha matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, Kuchunguza athari ya matumizi ya nyenzo katika kuchangia matokeo bora ya Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua na Kubainisha changamoto za matuimizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua. Sura hii pia imegawanywa katika sehemu mbili ambazo ni usuli wa watafitiwa na matokeo kulingana na madhumuni.

### 4.2Usuli wa Watafitiwa

Katika usuli wa watafitiwa, mtafiti alizingatia vipengele vifuatavyo: Umri wao, viwango vyao vya elimu na vipindi wanavyovifundisha kwa juma

#### 4.2.1. Umri wa walimu wa Kiswahili

Mtatifi alitaka kubaini umri wa walimu wanaofudisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.Matokeo ya maenezi ya umri wa walimu katika Jimbo la Nyandarua yanaonyeshwa katika jedwali 3 katika ukurasa ufuatao:

**Jedwali 3: Umri wa Walimu wa Kiswahili**

| Kijimbo | Sampuli kamili | Umri | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 16 -20 | 21 -25 | 26- 30 | 31 -35 | 36 -40 | 41 -45 | 46- 50 | Zaidi ya 50 |
| **Nyandarua Kaskazini** | 10 | 1 | 0 | 1 | 3 | 2 | 1 | 0 | 2 |
| **Mirangiini** | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| **Nyandarua Magharibi** | 6 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 |
| **Nyandarua Kati** | 7 | 0 | 0 | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| **Kipipiri** | 9 | 0 | 1 | 3 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 |
| **Nyandarua Kusini** | 5 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 |
| **kinangop** | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 2 |
| **Jumla** | 50 | 1 | 3 | 9 | 9 | 12 | 5 | 4 | 7 |
| **%** | | 2% | 6% | 18% | 18% | 24% | 10% | 8% | 14% |

Matokeo katika jedwali 3, yanaonyesha kuwa kiwango cha umri kati yamiaka 36 – 40, ndicho chenye idadi kubwa ya watafitiwa. Hii ikiwa ni asilimia 24%. Nacho kiwango 16 -20 kina asilimia 1% kikiwakilisha walimu wachache sana. Uchunguzi ulifichua kuwa walimu walio na umri wa miaka zaidi ya 50 katika Jimbo la Nyandarua ni asilimia 14%. Utafiti vilevile ulibaini kuwa, kijimbo cha Kinangop kina walimu wenye umri wa miaka 36 na kuendelea. Walimu walio na umri wa miaka 36 na kuendelea katika Jimbo la Nyandarua Magharibi ni asilimia 50%. Utafiti ukirejelea jedwali 3 unagundua kuwa kijimbo hiki (Nyandarua Magharibi) ndicho chenye matokeo bora zaidi katika Jimbo nzima la Nyandarua. Kutokana na matokeo haya, utafiti unaonyesha kwambakuna uhusiano wa matokeo bora na umri wa mtafitiwa.

### 4.2.2Viwango vya elimu vya walimu wa Kiswahili

Ili kubainisha ni kwa kiwango kipi kiwango elimu huathiri matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, mtafiti aliwaomba watafitiwa kujibu swali la 4 katika hojaji ya walimu. Matokeo haya yameonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4: Viwango vya Elimu ya Watafitiwa**

| Kijimbo | Sampuli kamili | Kiwango cha elimu | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | uzamili | % | Shahada | % | stashahada | % | Cheti cha ualimu | **%** |
| Nyandarua Kaskazini | 10 | 1 | 10% | 2 | 20% | 2 | 20% | 5 | 50% |
| Mirangiini | 6 | 1 | 16.67% | 1 | 16.67 % | 1 | 16.67 % | 3 | 50.00 |
| Nyandarua Magharibi | 6 | 1 | 16.67% | 1 | 16.67 % | 1 | 16.67 % | 3 | 50% |
| Nyandarua Kati | 7 | 1 | 14.29% | 1 | 14.29 % | 2 | 28.57 % | 3 | 42.86% |
| Kipipiri | 9 | 1 | 11.11% | 1 | 11.11 % | 1 | 11.11 % | 6 | 66.67% |
| Nyandarua Kusini | 5 | 0 | 0% | 1 | 20% | 1 | 20% | 3 | 60% |
| Kinangop | 7 | 1 | 14.29% | 1 | 14.29 % | 2 | 28.57 % | 3 | 42.86% |
| Jumla | 50 | 7 | 14% | 8 | 16% | 10 | 20% | 26 | 52% |

Kutokana na jedwali 4, matokeo yanaonyesha kuwa, walimu 7 (12.72%) wamehitimu katika kiwango cha uzamili ilhali Nyandarua Kusini haina mwalimu aliyehitimu katika kiwango hiki. Utatifi uliendelea kudhihirisha kuwa walimu 8 (16%) ndio waliohitimu katika kiwango cha shahada, nacho kijimbo cha Nyandarua Kaskazini kikiongoza katika kiwango hiki na walimu wawili. Walimu 10 (20%)wamefuzu katika kiwango cha stashahada. Vijimbo vya Nyandarua Kaskazini na Kinangop vinaongoza katika kiwango hiki kwa jumla ya walimu 2

katika kila jimbo. Uchunguzi ulionyesha kuwa, walimu wengi ambao wamehitimukatikakiwango cha cheti cha ualimu. Walimu hawa wamewakirishwa na asilimia 52%. Katika kiwango hiki, kijimbo cha Kipipiri kinaongoza kwa asilimia 66.67%, kikifuatwa na kijimbo cha Nyandarua Kusini kwa asilimia 60%. Kijimbo cha Kinangop ndicho chenye idadi ndogo ya walimu waliofuzu katika kiwango cha cheti cha ualimu. Katika kiwango hiki kijimbo cha Kinangop kimesimamiwa na asilimia 42.86%. Kwa jumla, walimu 24 (48%) wameboresha masomo yao kutoka yale ya cheti cha ualimu hadi ya kiwango cha uzamili. Killen (2006) anashauri kuwa taaluma zote, ikiwemo ya ualimu humhitaji mtaalamu kuyaimarisha masomo yake wakati wote atakaokuwa akifanya kazi ili apate maarifa na ujuzi mpya wa kuimarisha umilisi wake, hususan kwenye ufundishaji. Maoni yake Killen (2006) yanalingana na ya Gage (2009) anayeafiki kuwa, mwalimu wa kisasa aliyehitimu ni yule ambaye ameendeleza na kutumia vilivyo sayansi ya sanaa ya ujuzi na huwa na tajriba kamili ya ufundishaji. Isitoshe, mwalimu huyu hana budi kudhihirisha maarifa na ujuzi wa kutosha, tajriba ya kufundisha yenye umbuji ili kufaa mazingira bora ya ujifunzaji; zaidi ya hayo tajriba ya mwalimu iwe ya kufaa kwa kila kipindi na kwa kila kundi la wanafunzi. Kulingana na maoni ya watalamu hawa Killen (2006) na Gage (2009), inadhihirika kuwa mwalimu ambaye amepokea mafunzo ya kutosha katika taaluma ya ufundishaji ni yule mwenye ujuzi wa kutosha wa kutumia nyenzo wakati wa ufundishaji wake. Kutokana na jedwali 3, walimu wote wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane katika Jimbo la Nyandarua wamehitimu kuanzia kiwango cha cheti cha ualimu na kuendelea. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa walimu wa Jimbo la Nyandarua wana ujuzi wa kuteua na kutumia nyenzo faafu za kufundisha Kiswahili

### 4.2.3 Tajriba ya walimu wa Kiswahili.

Mtafiti alitaka kubaini iwapo tajriba ya walimu ina athari yoyote katika matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.Watafitiwa walijibu swali la5 katika hojaji ya walimu. Matokeo ya tajriba ya walimu yameonyeshwa katika jedwali, lifuatalo:

**Jedwali 5: Tajriba ya walimu wa Kiswahili**

| Miaka | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **0 – 5** | 4 | 8%% |
| **6 – 10** | 3 | 6% |
| **11 – 15** | 5 | 10% |
| **16 – 20** | 16 | 32% |
| **Zaidi ya 20** | 22 | 44% |
| **Jumla** | 50 | 100% |

Matokeo katika jedwali 5, yanaonyesha kuwa walimu 4 (8%) wana tajriba ya miaka 0 – 5.Nao walimu 3 (6%) wana tajriba ya miaka 6 – 10. Utafiti ulizidi kuonyesha kuwa walimu 5 (10%) wana ujuzi wa miaka kati ya 11 – 15. Walimu 16 (32%) wana tajriba ya miaka 16 – 20 na walimu 22 (44%) wana tajriba ya zaidi ya miaka 20. Lawrence (2005) anakiri kuwa tajriba ya ufundishaji ni muhimu ikitumiwa kama msingi wa kuendeleza taaluma ya ualimu kwani walimu wengi wanaimarisha matokeo ya kazi zao na kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika ufundishaji wao. Odera (2010)anasisitiza kuwa, mwalimu mwenye tajriba ni yule anayefanya maandalizi kabambe kabla ya kuingia darasani. Kutokana na matokeo ya jedwali 5, walimu wengi yaani 43 (86%) kati ya walimu 50, wana tajriba ya kutosha ya kuwawezesha kuteua na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.

### 4.2.4 Idadi ya vipindi wanavyofundisha walimu wa Kiswahili kwa juma

Mtafiti alitaka kubainisha idadi ya vipindi wanavyofundisha walimu wa Kiswahili kwa juma moja katika Jimbo la Nyandarua ili kubaini iwapo wanapata muda wa kutosha wa kutayarishanyenzo za kufundisha Kiswahili. Matokeo ya idadi ya vipindi wanavyofundisha walimu wa Kiswahili katika juma yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 6: Idadi ya Vipindi vya Kushughulikiwa na Walimu katika Juma**

| Vipindi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **0 – 5** | 0 | 0% |
| **5 – 10** | 0 | 0% |
| **11 – 15** | 2 | 4% |
| **16 - 20** | 3 | 6% |
| **Zaidi ya 20** | 45 | 90% |
| **Jumla** | 50 | 100% |

Kutokana na matokeo katika jedwali 6, ni wazi kwamba asilimia kubwa (90%) ya walimu ina idadi ya vipindi zaidi ya 20 kwa juma na kwa hivyo wanakosa muda wa kutosha wa kutayarisha nyenzo za kufundisha Kiswahili katika darasa lanane. Ni asilimia 10% ambayo inafundisha vipindi chini ya 20 kwa juma katika Jimbo la Nyandarua. Matokeo hayayanadhihirisha kuwa walimu wengi wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane wana kazi nyingi za kushughulikia hasa katika madarasa ya chini. Hata hivyo, mwalimu hana budi kujiandaa na kutayarisha nyenzo za kufundisha kabla ya kuingia darasani ili kufafanua dhana ngumu kwa urahisi na kuwa na athari chanya katika funzo lake. Lewis na Hill (1985) wanasisitiza kuwa maandalizi ya kina ni sharti yafanywe na mwalimu kabla ya kuingia darasani.

### 4.2.5 Ukaguzi wa hati za Kitaaluma

Mwalimu yeyote analazimika kutayarisha hati za kitaaluma kama inavyohitajika na taaluma ya ufundishaji. Hati hizo ni ratiba ya somo, andao la somo miongoni mwa nyingine. Walimu wakuu ndio wenye jukumu la kukagua hati hizi za kitaaluma. Ukaguzi ni njia moja ya kuimarisha ufundishaji wa somo lolote lile na kwa hivyo mtafiti alitaka kubaini ikiwa walimu wakuu wanakagua hati za kitaaluma. Matokeo ya ukaguzi huu yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 7: Miitiko ya Walimu Wakuu Kuhusu Ukaguzi wa Hati za Kitaaluma**

| Ukaguzi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Mara moja kwa mwezi** | 7 | 17.07% |
| **Mara mbili kwa mwezi** | 3 | 7.31% |
| **Mara moja kwa muhula** | 26 | 63.42% |
| **Mara kwa mara** | 5 | 12.19% |
| **Jumla** | 41 | 99.98% |

Kutokana na matokeo ya jedwali 8, imebainika kuwa, walimu wakuu 7 (17.07%) hukagua hati za kitaaluma mara moja kwa mwezi, walimu wakuu 3 (7.31%) hukagua mara mbili kwa mwezi, walimu wakuu 26 (63.41%) hukagua mara moja katika muhula ilhali walimu wakuu 5 (12.19%) hukagua mara kwa mara.

### 4.3 Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.

Ili kuinua kiwango cha matokeokatika somo la Kiswahili, mwalimu hana budi kutumia aina mbalimbali za nyenzo za kufundisha. Mtafiti alitaka kuchunguza nyenzo ambazo walimu waJimbo la Nyandarua hutumia wakati wa kufundisha somo la Kiswahili hasa katika darasa la nane. Watafitiwa walijibu swali la 7 katika hojaji ya walimu. Matokeo ya matumizi ya nyenzoza kufundisha Kiswahili yanadhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 8: Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili**

| | waliotumia | | Waliokosa kutumia | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nyenzo** | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | 50 | 100 % |
| **Ukuta/ubao mweusi** | 50 | 100% | - | - | 50 | 100 |
| **Picha** | 50 | 100% | - | - | 50 | 100 |
| **Vifaa halisi** | 45 | 90% | 5 | 10% | 50 | 100 |
| **Vifaa miigo** | 25 | 50% | 25 | 50% | 50 | 100 |
| **Projekta** | 19 | 38% | 31 | 62% | 50 | 100 |
| **Slaidi** | - | - | 50 | 100% | 50 | 100 |
| **Filamu** | 5 | 10% | 45 | 90% | 50 | 100 |
| **Ramani** | 13 | 26% | 37 | 74% | 50 | 100 |
| **Redio** | 39 | 78% | 11 | 22% | 50 | 100 |
| **Lebu za lugha** | - | - | 50 | 100% | 50 | 100 |
| **Tepe** | 3 | 6% | 47 | 94% | 50 | 100 |
| **Runinga** | 2 | 4% | 48 | 96% | 50 | 100 |
| **Tarakilishi** | 2 | 4% | 48 | 96% | 50 | 100 |

Kutokana na jedwali 8, matokeo yanabaini kuwa, walimu wote 50 (100%) hutumia ubao/ukuta mweusi na picha.Walimu 45 (90%) hutumia vifaa halisi. Vifaa miigo hutumiwa na walimu 25 (50%) ilhali walimu 25 (50%) hawavitumii. Utafiti ulionyesha kuwa, walimu 19 hutumia kadi za maneno. Hii ni asilimia 38 %. Projekta, slaidi na lebu za lugha hazitumiki na walimu wote 50. Hii ni asilimia (100%). Redio hutumiwa na walimu 39 ambayo ni asilimia (78%) lakini walimu 11, asilimia (22%) hawazitumii. Runinga hutumiwa tu na walimu 2 (4%) ilhali 48 (96%) hawazitumii. Silabasi mpya ya Kiswahili (2002) humhitaji mwalimu kukusanya nyenzo ambazo hutumika kuwasilisha uhalisia wa mambo darasani ili kupanua tajriba ya mwanafunzi kuhusiana na masuala mengi yanayomzingira yakiwemo maswala ibuka kama uadilifu, Ukimwi, mihadarati na uangamizaji wa uchochole. Naye Ngonga (2002) anasisitiza kuwa, picha husaidia katika utoaji wa mazoezi ya ufundishaji wa lugha hasa wakati wa kufundisha usomaji. Utafiti ulionyesha kuwa nyenzo za kimapokezi kama vile ubao na picha zingali zikitumika kwa wingi hata sasa. Nazo nyenzo za kisasa kama

vile, projekta, tarakilishi zinatumika kwa uchache mno. Slaidi na maabara ya lugha hazitumiki kamwe.

Aina za nyenzo ni nyingi, hivyo basi inambidi mwalimu kuteua na kutumia nyenzo katika kila kipindi. Utafiti unadhiririsha kuwa, ili ufundishaji wa Kiswahili uweze kuimarika na matokeo yapatikana katika mitihani ya Kitaifa katika Jimbo la Nyandarua, mwalimu hana budi kuteua na kutumia aina tofauti za nyenzo katika kila kipindi cha Kiswahili.

### 4.3.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundisha Kiswahili

Mtafiti alitaka kubaini njia ambazo walimu wa Jimbo la Nyandarua hutumia kuzipata nyenzo za kufundisha Kiswahili. Watafitiwa waliteua namna wanavyozipata nyenzo za kufundisha Kiswahlili. Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali 9, lifuatalo:

**Jedwali 9:Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundisha Kiswahili**

| | Idadi ya marudio | Asilimia % |
|---|---|---|
| **Ufadhili wa serikali** | 28 | 56 |
| **Uazimaji** | 2 | 4 |
| **Ufadhili wa wahisani** | 2 | 4 |
| **Ufaraguzi** | 5 | 10 |
| **Msaadawa wazazi/wanafunzi/mazingira** | 13 | 26 |

Kutokana na jedwali 9, matokeo yanaonyesha kuwa, walimu 28 (56%) walikubali kuwa nyenzo za kufundisha hufadhiliwa chini ya mpango wa serikali wa Elimu bila Malipo. Hata hivyo, ufadhili huu huwa hautoshelezi mahitaji ya nyenzo za kufundisha Kiswahili kikamilifu. Kutokana na upungufu huu, walimu hutafuta njia mbadala za kupata nyenzo za kufundisha Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalizidi kuonyesha kuwa, kati ya walimu 50 wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane wawili hufaragua nyenzo za kufundisha Kiswahili. Hii ni asilimia 4 %. Idadi ya walimu ambao hufadhiliwa na wahisani 2. Idadi ya walimu ambao hupata nyenzo za kufundisha Kiswahili kutoka kwa mazingira ni 13, hii ni asilimia 30%.

Njia hizi mbadala za kupata nyenzo za kufundisha Kiswahili yaani kuazima, kufadhiliwa na wahisani, kufaragua au kutoa kwenye mazingira, zinathibitishwa na miitiko ya walimu wakuu katika jedwali 10 kuhusu njia mbadala ambazo shule hufadhili nyenzo za kufundisha.

Jedwali 10: Njia Mbadala za Kufadhili Nyenzo za Kufundisha Kiswahili

| | **Idadi ya marudio** | **Asilimia %** |
|---|---|---|
| **Ufadhili wa wazazi** | 7 | 17.07 |
| **Uazimaji** | 6 | 14.63 |
| **Wahisani** | 3 | 7.31 |
| **Ufaraguzi** | 13 | 17.07 |
| **Mazingira** | 26 | 43.90 |

Kutokana na matokeo ya jedwali 10, ni wazi kuwa walimu wakuu vilevile hutafuta njia mbadala za kufadhili nyenzo za kufundisha. Idadi ya walimu wakuu wanaofadhiliwa na wazazi ni 7, hii ni asilimia 17.07%. Nayo jumla ya walimu wakuu 6 yaani asilimia 14.63 %, huazima nyenzo za kufundisha Kiswahili.


Asilimia 17.07% ya walimu wakuu, husaidia katika ufaraguzi wa nyenzo za kufundisha Kiswahili. Idadi ya walimu wakuu inayosaidia upatikanaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili kutoka kwa mazingira ni asilimia 43.90%.

Utafiti umedhihirisha kuwepo kwa upungufu wa nyenzo za kufundisha Kiswahili. Hata hivyo, asimilia 70% ya walimu wanaofundisha Kiswahili wamejimudu kufadhili nyenzo za kufundisha kupitia kwa njia mbadala kama vile kufaragua. Utafiti uliendelea kugundua kuwa, njia hizi za ufadhili huimarisha ufundishaji wa somo la Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.

### 4.4Viwango vya Matumizi ya Nyenzo za KufundishaKiswahili

Ili kufanikisha ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, mwalimu hana budi kuwa na mazoea ya utumiaji wa nyenzo za kufundisha. Mtafiti alitaka kufahamu viwango vya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua. Viwango hivi vilipimwa kulingana na mazoea ya utumiaji wa nyenzo za kufundisha Kiswahili. Watafitiwa wajibu swali la 8 katika hojaji ya walimu wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nane. Matokeo ya mazoea ya walimu dhidi ya matumizi ya nyenzo za kufundisha yanaonyeshwa katika grafu ifuatayo:

**Grafu1: Viwango vya Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili**




Viwango vya matumizi ya nyenzo vilipimwa katika mizani ya Likert ambapo nambari 1 ilionyesha mazoea ya kiwango cha juu zaidi, nambari 2 iliashiria mazoea ya kiwango cha juu. Nayo nambari 3 ilionyesha mazoea ya kiwango cha kadiri, nambari 4 ilionyesha mazoea ya kiwango cha chini ilihali nambari 5 iliashiria ukosefu wa mazoea. Kutokana na matokeo ya grafu1, ilibainika kuwa, ni walimu 3 wenye mazoea ya juu zaidi, hii ni asilimia 6% pekee. Walimu 4 ndio wenye mazoea ya juu, hii ikiwa ni asilimia 8%. Utafiti unaendelea kubaini kuwa, walimu 6 ndio wenye mazoea ya kadiri, hii ni asilimia 12 %. Walimu 5 ndio wenye mazoea ya kiwango cha chini, hii ni asilimia 10%.

Utafiti ulifichua kuwa walimu wengi hawana mazoea ya kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili. Matokeo yanaonyesha kuwa walimu 32 hawatumii nyenzo za kufundisha Kiswahili, hii ikiwa ni asilimia 64%. Abuli (2003) anarai kuwa, ukosefu wa matumizi ya nyenzo za kufundisha ni masikitiko makubwa sana kwa walimu ambao wanasisitiziwa kuhusu matumizi yake ili kiunua ujifunzaji na ufundishaji; pamoja na kuimarisha mazingira ya ujifunzaji. Utafiti ulionyesha kuwa walimu wengi hawatumii nyenzo za kufundisha Kiswahili kwa sababu moja au nyingine. Hata hivyo, utafiti unashikilia kauli kuwa ili ufundishaji wa Kiswahili uweze kuimarika na matokeo mema yapatikana, walimu wa Jimbo la Nyandarua hawana budi kuteua na kuwa na mazoea ya kutumia nyenzo za kufundishia.

### 4.4.1 Mbinu Za Matumizi ya Nyenzo za kufundisha Kiswahili

Baada ya mwalimu kuteua nyenzo, hana budi kuzitumia kwa njia inayofaa darasani ili kuathiri ufundishaji wake. Mtafiti alitaka kubaini jinsi walimu wa Jimbo la Nyandarua

hutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili. Watafitiwa walijibu swali la 8b katika hojaji ya walimu. Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali 11, lifuatalo**:**

**Jedwali 11: Mbinu Za Matuimizi ya Nyenzo za Kufundishia Kiswahili**

| Mbinu | Idadi | Asilimia |
| --- | --- | --- |
| **Maonyesho** | 50 | 100% |
| **Utandazaji** | 48 | 96% |
| **Utazamaji** | 50 | 100% |
| **Utumiaji wa kibinafsi** | 41 | 82% |
| **Utumiaji wa kimakundi** | 50 | 100% |

Kutokana na matokeo katika jedwali 11 ilidhihirika kuwa, walimu wote 50 hutumia mbinu ya maonyesho, mbinu ya utazamaji na mbinu ya kimakundi, hii ni asilimia 100%. Utafiti uliendelea kubaini kuwa, mbinu ya utandazaji hutumiwa na walimu 48. Hii ni asilimia 96%. Utafiti ulionyesha kuwa, walimu 41 huwashirikisha wanafunzi kibnafsi wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili, hii ni asilimia 82%. Kutokana na matokeo haya utafiti unashikilia kauli kuwa, ili kuimarisha matokeo ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, walimu hawana budi kuteua mbinu mwafaka wakati wa matumizi ya nyenzo.

### 4.5 Athari ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.

Nyenzo za kufundisha Kiswahili ni kiungo muhimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.Mtafiti alitaka kuchunguza athari za nyenzo za kufundisha Kiswahilikatika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua. Matokeo ya athari za matumizi ya nyenzo katika somo la Kiswahili yanadhihirika katika jedwali12.

**Jedwali 12: Athari ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundishia Kiswahili**

| Viwango vya Athari | Idadi ya marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| **Kiwango cha juu zaidi** | 12 | 24% |
| **Kiwango cha juu** | 20 | 40% |
| **Kiwango cha kadiri** | 11 | 22% |
| **Kiwango cha chini ya kadiri** | 4 | 8% |
| **Ukosefu wa athari** | 2 | 4% |
| **Ukosefu wa uhusiano** | 1 | 2% |
| **Jumla** | 50 | 100% |

Utafiti ulionyesha kuwa, walimu 12 (24%) waliafiki kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari ya kiwango cha juu zaidi katika ufundishaji wa Kiswahili. Nao walimu20 (40%) walikubali kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari ya juu. Walimu 11 (22%) walikubali kuwepo kwa athari za kadiri, walimu 4 (8%) wanaafiki kuwepo kwa athari fulani. Matokeo ya utafiti yalizidi kubaini kuwa, walimu 2 (4%) waliamini kutokuwepo na athari zozote ilhali mwalimu 1 (2%) hakupata uhusiano wowote wa nyenzo na ufundishaji wa Kiswahili.

Utafiti uligundua kuwa nyenzo za kufundisha zina athari nyingi katika ufundishaji wa Kiswahili.Moja ya athari hizi ni kuinua kiwango cha mwanafunzi cha kushiriki darasani. Athari hii inasisitizwa na Suleimani (1998) anapodai kuwa vifaa vya kufundisha huwa ni daraja kati ya funzo na mawazo ya mwanafunzi na zaidi huchochea ushirikishwaji wa mwanafunzi darasani.

Walimu 41(82%) walikubali kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili huwapa wanafunzi umilisi wa maongezi na wa kimaandishi. Matokeo haya yanahusiana na yale ya Wright (1989) ambayo yanasisitiza kuwa, nyenzo za kuonwa hutumika vyema kufunzia usikilizaji, usomaji,uandishi, uzungumzaji,sarufi na kaida za lugha na hivyo kuwapa wanafunzi umilisi wa lugha. Utafiti ulibaini kuwa, walimu 35 (70%) wanaafiki kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili huzidisha uwezo wa mwanafunzi wa kuingiliana vyema na tajriba yake. Maoni haya yanalingana na maoni ya Dales (1999) anapodai kuwa, nyenzo za kufundisha humpa mwanafunzi tajriba yenye mguso na zaidi humwezesha kuingiliana vilivyo na tajriba yake.

Utafiti uliendelea kuonyesha kuwa, nyenzo za kufundisha Kiswahili huchunga muda na hivyo humfanya mwalimu kuwa mdhibiti bora wa kipindi. Matokeo haya yanahusiana na maoni ya Brown (1993) anaposisitiza kuwa, dhima kuu ya nyenzo za kufundisha ni kuokoa muda, kuchochea shauku na kumpa mwanafunzi motisha wa kushiriki katika kipindi.Utafiti unaonyesha kuwa walimu 43 (86%) walikubali kuwa nyenzo za ufundishaji wa Kiswahii katika Jimbo la Nyandarua zinachangia mno katika ufundishaji wa Kiswahili. Kutoka na matokeo haya, utafiti unashauri kuwa mwalimu wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua hana budi kutumia nyenzo za ufundishaji ili ainue kiwango cha matokeo ya Kiswahili katika shule za msingi za umma.

### 4.6 Changamoto za Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili

Utafiti ulitaka kuchunguza kuhusu changamoto zinazowakabili walimu wanaofundisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua wakati wa matumizi ya nyenzo za ufundishaji. Kwa hivyo, watafitiwa walijibu swali la 10 katika hojaji ya walimu. Matokeo yanaonyeshwa katika lifuatalo.

**Jedwali 13: Changamoto Za Matumizi ya Nyenzo za Kufundisha Kiswahili.**

| Changamoto | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| **Upungufu wa nyenzo** | 28 | 56% |
| **Ukosefu wa fedha** | 25 | 50% |
| **Upungufu wa wakati** | 47 | 94% |
| **Ukosefu wa ujuzi wa kutosha** | 8 | 16% |
| **Mitazamo hasi** | 13 | 26% |
| **Maandalizi duni** | 5 | 10% |

Matokeo katika jedwali 13yanaonyesha kuwa, walimu 28 walikubali kuwepo kwa upungufu wa nyenzo za kufundisha Kiswahili, hii ikiwa ni asilimia 56%. Walimu 25 walilalamikia ukosefu wa fedha za kutosha za kununua nyenzo za kufundisha Kiswahili, hii ni asilimia 50%.Utafiti uliendelea kubaini kuwa, walimu 8 walikubali kuwepo kwa upungufu wa tajriba ya kutosha kuhusiana na matumizi ya nyenzo za kufundishia, hii ikiwa ni asilimia 16%.Nao walimu 13 walikubali kuwa na mitazamo hasi kuhusu nyenzo za kufundisha. Hii ni asilimia 26%. Walimu 5 wakiri kuwa na maandalizi duni, hii ikiwasilishwa ni asilimia 10%.

Kulingana na utafiti huu, changomoto kubwa ya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni ukosefu wa wakati wa kutayarisha nyenzo. Changamoto hii imesimamiwa na walimu 47, hii ni asilimia 94%. Matokeo haya yanahusiana na mapendekezo ya Chuo Kikuu cha St Cloud (2009), nchini Marekani kuhusu hatua za kuzingatiwa na walimu kabla ya kuteua nyenzo za kufundisha. Miongoni mwa hatua hizo ni kule kutafuta muda wa kutayarisha nyenzo ya kufundisha. Kutokana na chanagamoto hii, utafiti unashauri kuwa, ili kupatikane matokeo mazuri katika mtihani wa kitaifa, mwalimu hana budi ila kutafuta muda zaidi wa kutayarisha nyenzo za kufundisha.

Utafiti uligundua kuwa asilimia 50% ililalamikia ukosefu wa fedha za kufadhili nyenzo za kufundisha Kiswahili. Kutokana na changamoto hii, Strauss na Frost (1999) wanamshauri mwalimu kuteua nyenzo ambayo taasisi inaweza kumudu gharama yake.

Utafiti uliweka wazi kuwa asimilia 16% ya watafitiwa ilikubali kuwa na upungufu wa tajriba ya kutosha ya kutayarisha na kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili. Kutokana na changamoto hii, ndipo wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Missouri (2012) wanamsisitizia mwalimu kuwa na tajriba ya kutosha ya kutumia nyenzo za kufundisha.

Utafiti umebaini kuwa changamoto zinazowakabili walimu wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni nyingi. Hata hivyo, utafiti unashikilia kuwa ili kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua, mwalimu wa Kiswahili hana budi kukabiliana na changamoto za matumizi ya nyenzo.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia: Muhtasari wa utafiti, hitimisho la utafiti, mapendekezo ya utafiti na mapendekezo ya tafiti za ziada.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua,Kenya. Mada hii ilichambuliwa kupitia kwa wataalamu mbalimbali ili kubaini uhalali wake. Matini mbalimbali zilipitiwa katika mapitio ya maandishi kulingana na madhuni ya utafiti. Katika sura ya tatu utafiti ulizua mbinu za kukusanya data ya utafiti. Muundo wa kimaelezo ulitumika katika utafiti huu. Kifaa kikuu cha ukusanyaji wa data kilikuwa hojaji.

Baada ya kuchanganua matokeo kulingana na madhumuni ya utafiti, utatifi ulibaini kuwa kuwa walimu walio na umri wa kati ya miaka 36 – 40 ndio wengi kwa asilimia 24%. Kisha utafiti ulionyesha kuwa walimu waliofuzu katika cheti cha ualimu cha P1 ndio wengi kwa asilimia 52%. Utafiti pia ulichunguza tajriba ya walimu katika ufundishaji wa Kiswahili. Iliibuka kuwa asilimia 86% ina tajriba ya zaidi ya miaka 11. Utafiti pia ulifahamu kuwa asilimia 82% ya walimu ina zaidi ya vipindi 30 katika kila juma. Utafitiulifichua kuwa walimu hutayarisha hati za kitaaluma kwa kila muhula. Asilimia 63.41% ya walimu wakuu hukagua hati za kitaaluma mara moja kwa kila muhula.

Utafiti uligundua kuwa walimu 32 (64%) walikubali kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari kuu katika ufundishaji wa Kiswahili. Isitoshe, nyenzo hizi huwa na athari chanya kwa mwanafunzi. Ni mwalimu mmoja tu 1 (2%) aliyedai kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili hazina athari yoyote kwa mwanfunzi.

Utafitiulibaini kuwa, walimu wote 50 (100) hutumia ubao/ukuta mweusi na picha. Vifaa halisi hutumiwa na walimu 45 (90%), nayo redio hutumiwa na walimu 39 (78%). Vifaa miigo hutumika kwa kiwango cha wastani ya asilimia 50%. Nyenzo ambazo hutumika kwa uchache

ni filamu kwa asilimia 10%, tepe asilimia10%, runinga kwa asilimia 24% na tarakilishi kwa asilimia 4%. Nyenzo za kisasa kama vile slaidi na projekta hazitumiki. Hii ikisimamiwa na asilimia 100%

Utafiti ulifichua kuwa walimu 32 (64%) hawana mazoea ya kiwango cha juu katika matumizi ya nyenzo za ufundishaji wa Kiswahili. Utatifi uligundua kuwa walimu hutumia mbinu mwafaka wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha. Kwa mfano, mbinu ya maonyesho na utandazaji hutumiwa na walimu wote wa jimbo. Hii ikiwa asilimia 100%

Changamoto zinazowakuba walimu wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili ni nyingi. Changamoto kuu ikiwa ni ukosefu wa muda wa kutosha wa kuandaa nyenzo za kufundisha. Changamoto hii ikiwakilishwa na asilimia 94%. Walimu wengi walilalamikia mrudiko wa kazi nyingi kama kizuizi kikuu cha kutoshughulikia nyenzo za ufundishaji wa Kiswahili.

**5.3 Hitimisho**

Baada ya kukamilisha utafiti kuhusu matuimizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili, utafiti ulihitimisha kuwa:

i) Walimu wa Jimbo wanatumia aina tatu za nyenzo ila kwa upungufu. Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa matumizi ya vifaa vya kisasa kama vile tarakilishi/vipakatalishi 4%, runinga 4%, filamu 10%, kanda za kunasia sauti 6% na slaidi 0%.

ii) Zaidi ya asilimia 64% ya watafitiwa iliafi kuwa na mazoea ya kiwango cha chini cha matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili.

iii) Asilimia 68% ya watafitiwa iliafiki kuwa nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari kuu katika kufanikisha ufundishaji wa Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua.

iv) Asilimia 94% ilisuta ukosefu wa muda kama kizuizi kikubwa cha ukosefu wa maandaliziya nyenzo za kufundishia Kiswahili

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Ili kuboresha matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za umma katika Jimbo la Nyandarua, utafiti ulizua mapendekezo yafuatayo:

i) Ili kuwa na umilisi wa matumizi nyenzo, utafiti unapendekeza kuwa serikali iwaandaliye walimu wa Kiswahili warsha na semina ili wapate maarifa na ujuzi wa kutumia hususani nyenzo za kisasa kama vile tarakilishi na mitandao. Serikali kupitia kwa Wizara ya elimu na Taasisi ya Kukuza Mitaala nchini ianzishe vituo vya nyenzo za kufundisha Kiswahili kuanzia mashinani hadi katika ngazi za kitaifa.

ii) Ili kuinua kiwango cha matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika Jimbo la Nyandarua utafiti unapendekeza njia za kisasa kama vile matumizi ya projekta, lebu za lugha na matumizi ya teknolojia ya kisasa zishirikishwe ili kuwapa walimu motisha wa kutumia nyenzo za kufundisha Kiswahili.

iii) Ili kuathiri ufundishaji na ushirikishwaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili, mwalimu hana budi kutumia nyenzo kila wakati anapofundisha ndani au nje ya darasa.

iv) Ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili walimu wakati wa matumizi ya `nyenzo za kufundisha, utafiti unapendekeza ushirikiano wa walimu, serikali, wanafunzi za wahisani wengine wa sekta ya elimu katika kuandaa nyenzo ili mwalimu atumie muda vizuri. Zaidi utafiti unapendekeza kuanzishwa kwa maktaba ya nyenzo za kufundisha Kiswahili katika kila shule ya msingi ya umma katika Jimbo la Nyandarua.

## 5.5 Mapendekezo Kuhusu Utafiti wa ziada

Utafiti umegundua kuwa walimu wengi wana udhaifu wa kutumia nyenzo za kufundisha hasa nyenzo za teknolojia ya kisasa.Kwa hivyo, kuna haja ya tafiti kufanywa katika sehemu zifuatazo;

i) Ujuzi wa walimu kuhusiana na nyenzo zinazotumia teknolojia ya kisasa.

ii) Utafiti sawia kufanywa katika sehemu zingine hapa nchini Kenya

## MAREJELEO


Abuli, W. O. (2003).*An Evaluation of the Extent to which Audio visual and visual media Are Used for instruction: A case study of Lusengeli secondary schools in Vihiga County, Western Region.*Unpublished Mph Moi University.

Aduwa,O. & Iyamu, S. E. (2009). *Factor affecting quality ofEnglish language teaching learning in secondary schools in Nigeria:*Unpublished PHD Thesis: University of Benin: Benin city, Nigeria.

Anderson, R. W. & Krathwohl, J. K. *Selection and Development of Media for instruction*. .New York: Van Nostrand.

Brown, J. (1993). *Audio visual Instruction Techniques, Media, and Methods*. New York : Mc Graw- Hill, Inc.

Callahan, J.K. (1992). *Teaching in Middle and Secondary Schools*. New York. Macmillan Publishers Co., Inc.

Dales, E. (199). *Audio Visual Methods in Teaching*. New York: Holt, Renehalt, and Winston, Inc.

Bruner,J. (1996). *Toward a Theory of Instruction*. New York: Harvard University Press.

CHAKITA. (2012). *Uamilifu wa Makala za Taifa Leo Kama Nyenzo za Kufundishia Kiswahili*. www. Chakita. Org. ./ chakita- program. Pdf .

Cohen, M, & Manion, C. (2000). *Research Methods in Education:* London:Croomhelm.

Copper, H. (1998). *Aids to Teaching and Learning*. New York: Pergamon Press.

Daft, R.L. & Lengel, R. H. (1986). *Information Richness: a New Approach to Managerial Behavior and Organizational Design.* Cummings, L.L. Staw, B.M. (Eds), Research in zational behavior 6, (191-233). Homewood, IL:JAI Press.

Deuter, M., Bradbery, J.& Turnbull, J. (2015). *Advanced Learner's Dictionary International Student's Edition:* London: Oxford University Press.

Ellis,R. (1999). The Empirical Evaluation of Language Teaching material:ELT Journal. *Vol 5,* No.1 pp112-119.

El- Shinnaway, D.K., Maha, M., & Lynne, M. (2009). "The Poverty of Media Richness Theory: Explaining People's choice of electronic vs voice mail*". International Journal of Human Computer Studies* 46 (4): 443- 467. doi: 10.1006/ijh.2010.009.

Flanders, N. A (1970). *AnalyzingTeaching Behaviour*. New York: Addison-Wesley co.

Finocchiaro, M. (1993). *The Foreign Language Learner. A Guide for Teacher*. New York: Regents Publishing Company, Inc.

Gage, N. (2009). *Educational Psychology:* Chicago Rand and Mc Nally Education.

Gall, M. D., Borg, W. R . & Gall, J. P. (2007). *Educational Research: An introduction*. New York: Longman Publishers.

Gay, H. (1983).*Educational Research: Competences for Analysis and Application*. London: Charles. E. Merill publishers.

Gathumbi,A. W., & Ssebbunga, C. M. (2005).*Principles and Techniques in language Teaching; A Text for Teacher Educators. Teachers and Pre-service Teachers,* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Heinrich, R. (1993*). Instruction Media and The Technology of Instuction.* New York: Macmillan Publishers

Joyce, P. J., Gall, M. D., &Walter, R. Borg. (1996). *Educational Research: An Introduction (8th Edition)*New York: University of Oregon Publishers.

Kasbolah, K. (2003). *Teaching-Learning Strategy*. Malang: IKIP Malang.

Kathuri, N. J.& PALS, D. A (1993). *Introduction to Educational Research*. Nakuru: Egerton University Press.

Kock, N. (2005). "Media Richness Media Naturalness? The evolution of our biological. apparatus and its influence on our behavior toward e-communication tools". *IEEE Transactions on Professional Communication* 48 (2):117- 130.doi:10.1109/tpc.2005

Kombo, D. K. & Tromp, D.L (2006). *Proposal and Thesis Writing. An introduction.* Nairobi:Pauline Publication.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*: *MethodsandTechniques*: New Delhi NewAge International (p) Ltd.

Lee, O. (2000). The Role of Cultural Protocol in Media Choice in a Confucian Virtual Workplace*".IEEE Transactions on Professional Communication* 43 (2): 196.doi:10.1109/47.843646.

Lewis, M., &Hill, J (1985). *Practical Techniques for Language Teaching.*Howe: LanguageTeaching Publications.

Luvisa, J. C. 2003). *Availability and Use of Instructional Resources in TeachingKiswahili Grammar in Secondary Schools in Bungoma District.* Unpublished Mph MoiUniversity.

Markus, M.L. (1994). “Electronic Mail as the Medium of managerial Choice”.*Organization Science **5*** **(**4): 502-527.doi:1287/orsc.5.4.502. JSTOR 2635179.

Mbuthia, F. (1996). *A Comparative Study of Effects of two Instructional Methods of students Performance in Kiswahili writing lessons in Eldoret Municipality*.Unpublished Med Thesis: Moi University.

Mdee, J. S., Njogu.,& K., Shafi, A. *(2014). Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mugenda,O. M.and Mugenda, A. G. (2003*). Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Africa Centre for technology studies (ACTS) press.

Ngwenyama, K. Ojelanki, K. & Allen, S. (`1997). Communication Richness in Electronic mail: Critical Social Theory and the Contextuality of Meaning. *MIS Quarterly* 21 (2): 145-167. doi: 10.2307/249417. JSTOR 249417.

Ngonga, B. (2002). *An Assessment of English Language Teacher Education in The Light of Classroom Needs:A Case Study of Masemo University:*Unpublished Thesis: Maseno University.

Odera, F. Y. (2010).*School Radio Programmes: A Case Study of Its Use in Selected Institutions in Nyanza Region in Kenya.* MpHil Thesis Wales Great Britain.

Okwako, R. (1994). *A Survey of Resources Available for Teaching Reading in English in Secondary schools in Kenya.*Unpublished M.Ed Thesis: Eldoret: Moi University.

Oldham.(2012). *Resources for the Oldham County School media center LMS*. Retrieved from http://www.ala.org/booklist.

Republic of Kenya, Ministry of Education, (2002*). Primary Education Syllabus vol 2.* Kenya Institute of Education.

Republic of Kenya. (1964) . *Report of the Ominde Commission of Kenya*.

Roy, K. (2006). *Effective Teaching Strategies Lessons from Research and Practice:* Cengage Learning Centre: Australia.

Romiszowiski, A. J. (1988). *The selection and use of Instructional Media:* Kogan Page Publishers.

Schullstorm, F.(1998). *Guidelines or selection of materials in English language arts program.* NCTE 1111 W. Kenyon Road, urbana Illinois 61801-1096. Retrieved from www.ncte.org/../selecting ela materials.

St Cloud State University. (2012). *Developing Support Materials*. Accessed (2012) at http://irs.st.cloudsstate.edu/cim/courses/pine/develop.html

Sugiharto, W. (1994). *The Use of Visual Media in Teaching of English in Junior High School in Kodya Malang.* Unpublished Thesis. Malang: FPBS IKIP Malang.

Suleimani, A. H. (1998) *Media Audio – Visual. Pengajara*: PT. Gramedia.

University of Missouri-Columbia (2012), *School of Information Science and learning Technologies choosing a Technology mix for Distance Education*. http://web.pdx.edu/mmlnch/media selection 3 docRetrieved 20/03/2013

William, M. K. (2001). *The Research Methods Knowledge Base*. Newyork: Dog Publishers.

Wringe, C. (1995). *The Effective Teaching of Modern Teaching Languages UK*:

Longman Group Ltd.

Zacharia, U. (2012 . *Maandalizi ya Ufundishaji*. Dar es Saalamu: LuwinguWordpres

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A

### HOJAJI YA WALIMU WA KISWAHILI

Madhumuni ya hojaji hii ni kukusanya data kuhusu *matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, Jimbo la Nyandarua, Kenya***.** Tafadhali jibu maswali yafuatayoili kunisaidia katika utafiti huu. Ninakuhakikishia kuwa usiri wa kiwango cha juu utazingatiwa na kuwa miitiko yote itakayotolewa hapa haitatumika kwa njia nyingine ile isipokuwa kwa madhumuni ya utafiti huu**.** Weka kikwaju ( √ ) iwapo panahitajika hivyo.

**<u>SEHEMU A: USULI WA MTAFITIWA</u>**

1. Jina la shule …………………………………………………..
2. Je, shule yako iko katika kijimbo kipi cha Jimbo la Nyandarua?
   *Nyandarua Kaskazini (   ) Mirangi-ini (   ) Nyandarua Magharibi (   )*
   *Nyandarua Kati (   ) Kipipiri (   ) Nyandarua Kusini (   ) Kinangop (   )*
3. Una umri wa miaka mingapi?

   16 – 21 ☐ 21 – 25 ☐ 26 – 30 ☐ 31 -35 ☐ 36 – 40 ☐ 41 -45 ☐

   46 - 50 ☐ 51 -55 ☐ 56 -60 ☐

4. Kiwango cha juu cha elimu.

A) Uzamili ☐ B) shahada ☐ C) stashahada ☐ D) cheti cha ualimu ☐

5. Je, umefundisha Kiswahili katika darasa la nane katika shule za msingi za umma kwa muda wa miaka mingapi?
   0- 5 ☐ 6 -10 ☐ 11- 15 ☐ 16 – 20 ☐ zaidi ya miaka 20 ☐
6. Unafundisha vipindi vingapi kwa juma?
   0 - 5 ☐ 6 – 10 ☐ 11- 15 ☐ 16 – 20 ☐ zaidi ya 20 ☐

**SEHEMU B: MATUMIZI YA NYENZO ZA KUFUNDISHA KISWAHILI.**

7a) Je, ni nyenzo zipi unazotumia mara kwa mara wakati wa kufundisha Kiswahili?

| | | |
|---|---|---|
| Nyenzo za kuonwa | Ubao/ukuta mweusi | ☐ |
| y | Picha | ☐ |
| e | Vifaa halisi | ☐ |
| n | Vifaa miigo | ☐ |
| z | Chati | ☐ |
| o | Kadi umeme | ☐ |
| | Projekta | ☐ |
| z | Slaidi | ☐ |
| a | Filamu | ☐ |
| | Ramani | ☐ |
| k<br>Nyenzo za kusikilizwa<br>u | Santuli | ☐ |
| f | Tepu rekoda | ☐ |
| u | Lebu za lugha | ☐ |
| n | Redio | ☐ |
| d | Tepe | ☐ |
| i | Kanda (CD/DVD) | ☐ |
| s Nyenzo za kusikilizwa/kuonwa | Runinga/video | ☐ |
| h | Tarakilishi | ☐ |
| a | Kanda (DVD) | ☐ |
| | Ipadi | ☐ |
| | Slaidi za filamu | ☐ |

b)

Nyenzo za kufundisha hupatikana kwa njia nyingi. Teua njia unayoitumia auunazozitumia

kupata nyenzo za kufundisha Kiswahili katika shule yako.

Ufadhili chini ya mpango wa serikali wa Masomo bila Malipo (MbM) ☐

Uazimaji ☐ ufadhili wa wahsani ☐ ufaraguzi ☐ mazingira ☐

8a)Ili ufanisi wa ufundishaji upatikane, mwalimu hana budi kuwa na kiwango cha mazoea

ya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Tia kikwaju ( √ ) panapohitajika.

Mazoea ya kiwango cha juu sana ☐

Mazoea ya kiwango cha juu ☐

Mazoea ya kadiri ☐

Mazoea ya chini ya kadiri ☐

Ukosefu wa mazoea ☐

b) Zifuatazo ni mbinu zinazotumiwa na walimu wakati wa matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Kwa kutia kikwaju ( √ ), teua mbinu unazozitumia.

Maonyesho (  ) utandazaji (  ) matumizi ya projekta (  ) utumiaji wa kibinafsi (  ) utumiaji wa pamoja- kimakundi (  )

c) Iwapo kuna mbinu zingine uzitumiazo, tafadhali fafanua

………………………..…………………………………

9a) Je, nyenzo za kufundisha Kiswahili zina athari yoyote katika kufikia sabaha ya funzo katika kipindi?

Ndio ☐ La ☐

b) i) Iwapo jibu lako ni ndio, kwa kufuata mizani iliyotolewa hapo chini, teua jibu lifaalokwa kuweka kikwaju ( √ ) 1= nakubali kabisa, 2= nakubali, 3= sina uhakika, 4= sikubali, 5=sikubali kabisa.

| **Athari ya matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili** | **Kiwango cha makubaliano** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| a) Kiwango cha mwanafunzi cha kushiriki darasani huimarika | | | | | |
| b) Kumbukizi huimarika | | | | | |
| c) Vifaa vya ufundishaji huchochea shauku ya mwanafunzi | | | | | |
| **d)** Mwanafunzi huchangamkia kipindi | | | | | |
| **e)** Mwanafunzi hupata umilisi wa maongezi na wa maandishi | | | | | |
| **f)** Mwanafunzi huingiliana vyema na tajriba yake | | | | | |

ii) Je, nyenzo za kufundisha zina athari zingine zozote?

Ndio ☐ La ☐

iii) Iwapo jibu lako ni ndio, fafanua……………………………………………

10 a) Zifuatazo ni changamoto za matumizi ya nyenzo za kufundisha Kiswahili. Kwa kutia kikwaju (√ ) panapohitajika, chagua jibu lifaalo.

Ukosefu wa nyenzo ( ) ukosefu wa fedha ( ) upungufu wa wakati ( ) upungufu wa ujuzi ( ) mtazamo hasi kuhusu matumizi ya nyenzo ( ) maandalizi duni ( ).

b) Iwapo kuna changamoto zingine zinazokukabili, tafadhali zielezee……………………….

………………………………………………………………………………………

**KIAMBATISHO B**

**HEAD TEACHERS' QUESTIONNAIRE**

The purpose of this questionnaire is to collect data on *the utilizationof instructional media in teaching of Kiswahili in public primary schools, Nyandarua County*. Kindly take time to respond to all questions as honestly and accurately as possible. All responses will be treated with confidentiality. Please tick ( √ ) against information(s) most applicable.

**SECTION A: General information of respondent**

1. In which of the following sub-counties is your school located? Tick as appropriate.

*Nyandarua North ( ) Mirangi-ini ( ) Nyandarua West ( ) Nyandarua Central ( )*

*Kipipiri ( ) Nyandarua South ( ) Kinangop ( )*

***2.*** What is the average number of lessons each teacher takes in a week in your school?

0 – 5 ☐ 6 – 10 ☐ 11 -15 ☐ 16 – 20 ☐ 21 – 252☐0 ☐

Over 30 ☐

3. (i) Do teachers in your school prepare:

Schemes of work?

Yes ☐ No ☐

Lesson plans? Yes ☐ No ☐

Teaching aids Yes ☐ No ☐

(ii) How often do you assess whether teacher(s) use teaching aids specifically in teaching of Kiswahili in class eight?

Once a month ☐ twice a month ☐ once a month ☐ once a term ☐

Once a year ☐ never ☐

**SECTION B: UTILIZATOIN OF INSRUCTIONAL MEDIA IN KISWAHILI**

4. What kind of media is often used by Kiswahili teacher(s) in class eight in your school?

| | | |
|---|---|---|
| Visual aids | Black board/wall | ☐ |
| | Pictures | ☐ |
| | Real objects | ☐ |
| | Realia | ☐ |
| | Charts | ☐ |
| | Flash cards | ☐ |
| | Slides | ☐ |
| | Films | ☐ |
| | Maps | ☐ |
| Audio aids | Tape Recorder | ☐ |
| | Laboratory Language | ☐ |
| | Redio | ☐ |
| | CD/DVD | ☐ |
| Audio visual aids | Internet | ☐ |
| | Tapes | ☐ |
| | Video | ☐ |
| | Computer | ☐ |
| | I pad | ☐ |
| | Slides | ☐ |
| | Television | ☐ |

(i) Does the government cater fully in provision of instructional media specifically in Kiswahili?

Yes ☐ No ☐

(ii) If your option is a no, how does your school supplement?

Parents' funding ☐

Borrowing ☐

Donors/wellwishers ☐

Others specify………………………………………………………………

5a) What is the frequency of utilization of instructional aids in teaching of Kiswahili in class eight in your school?

Very high frequency…………………………………... ☐

Above average………………………………………….. ☐

Average……………………………………………… ☐

Below average………………………………………. ☐

b) The following are methods used by Kiswahili teachers in utilization of an instructional media in a classroom situation. Tick ( √ ) as appropriate.

Demonstration ( ) displaying on soft boards ( ) projection ( ) direct observation ( ) individual manipulation ( ) others specify……………………………………………

6 Use a tick ( √ ) against the correct option as per the scale provided below, indicate the effects of an instructional media on lesson's objective(s) in Kiswahili?

1= strongly agree, 2= agree, 3= don't agree, 4= disagree, 5= strongly disagree.

| **Effects of instructional media** | **Level of agreeableness** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| pupils' participation in class is enhanced | | | | | |
| pupils' retention power improve | | | | | |
| Pupils are motivated | | | | | |
| Pupils interact with prior experience easily | | | | | |
| Pupils' competence level in spoken/written improve | | | | | |
| pupils'performance generally improve | | | | | |
| No effects | | | | | |

Others specify…………………………………………………………………...

7. The following are some challenges facing Kiswahili teachers in utilization of instructional media. Choose an appropriate option by placing a tick ( √ ) against it.

Inadequancy (   ) Lack of funds (   ) Scarcity of time (   ) Poor/ lack of preparation by teachers (   ) Lack of experience (   ) Negative attitude by teachers (   )

Others specify……………………………………………………………………………………

8. In your own opinion, what do you think should be done to improve utilization of Kiswahili instructional media in Nyandarua County?....................................................................................

…………………………………………………………………………………………………

## KIAMBATISHO D

## BARUA YA MAPOKEZI

KARIUKI P.M.

S. L. P. 249,

MIHARATI.

Kwa mjibu,

KUH: HOJAJI

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara, idara ya Mitaala na Mbinu za Ufundishaji. Baadhi ya mahitaji ya kozi hii ni kufanya utafiti na kuandika tasnifu. Mada ya Utafiti wangu ***'Matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, Jimbo la Nyandarua*'.**

Naomba usaidizi wako kwa kujaza hojaji hii ili kuniwezesha kukusanya data inayohitajika. Nakuhakikishia kuwa miitiko yote utakayoitoa itatumika tu kwa madhumuni ya utafiti huu na kuwa usiri wa kiwango cha juu utazingatiwa.

Wako mwaminifu

Kariuki P. M